BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,010,689,585/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Miaka** 60 ya Uhuru wa Burundi na ndoto za kuwa shirikisho

UKURASA 4



**SHILOLE UNATAKA KUMTIBUA BABA LEVO**

UKURASA 20


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Julai 3, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-


ISSN 0856 • No. 0580995

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Athari hasi wanandoa kuishi mbali na familia

UKURASA 8





Watoto, wanawake waathirika namba moja



Ni sehemu ya maficho ya 'panya road'



Kiini cha michepuko, ufanisi duni kazini



Mtaalamu ataka maboresho ya sheria

## YALIYOMO


UKURASA WA 3

**WAJIFUNGULIA GETINI, WATUMISHI ZAHANATI WASIMAMISHWA KAZI**

WATUMISHI watatu wa Zahanati ya Kashai iliyoko Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera, Reticia Muganyizi (45), Binkwaya Haruna...

UKURASA WA 3

**POLISI WADAIWA KUKATAA KUFANYA UCHUNGUZI**

ASKARI wa Kituo cha Polisi Misigiri katika Wilaya ya Iramba mkoani Singida wanadaiwa kukataa kufanya uchunguzi wa...

UKURASA WA 5

**NEMC YABAINI TATIZO LA KEMIKALI KIWANDA SUKARI**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limefanya ziara ya kushtukiza katika Kiwanda cha Sukari cha Mtibwa...


## Serikali yatoa kauli 150,000 waliokosa ajira zake

UKURASA 2



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na waandishi na wahariri wa vyombo vya habari, Ikulu, jijini Zanzibar jana, kuhusu masuala mbalimbali ya maendeleo ikiwamo miundombinu na utalii. **PICHA: IKULU**

## Dk. Mwinyi akasirishwa na taarifa za upotoshaji

UKURASA 2

MICHEZO | YANGA SC BINGWA FA UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akimsikiliza Kamishina Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Gerald Kusaya (wa pili kushoto), wakati alipotembelea banda la Taasisi ya Walter Reed Army Institute of Research (WRAIR), katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kupinga Matumizi ya Dawa za Kulevya Duniani yaliyofanyika kitaifa kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: OWM**

# Serikali yatoa kauli 150,000 waliokosa ajira

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imewataka waombaji 149,272 waliokosa ajira za ualimu na kada za afya zilizotolewa hivi karibuni, kuwa wavumilivu kwa kuwa ajira zingine zitaendelea kutangazwa.

Hivi karibuni, Serikali ilitangaza kuajiri watumishi wapya 16,676 wa ajira za ualimu na kada za afya kati ya 165,948 waliokuwa wameomba ajira hizo.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, alibainisha hayo jana jijini alipofungua kikao kazi cha Maofisa Uhusiano wa Taasisi na Maofisa Habari wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Alisema ajira zimezingatia vigezo vyote na wamesimamia haki na ushindani ulikuwa mkubwa.

"Asilimia 10 ya walioomba wamepata na asilimia 90 na wao walitamani kupata lakini hawakupata, wito wangu waendelee kuwa wavumilivu, ajira zitaendelea kutangazwa," alisema.

Waziri huyo pia alisema nafasi za ajira 736 hazikupata walengwa sahihi kutokana na walioziomba kutokukidhi vigezo, hivyo zitatangazwa upya hivi karibuni.

"Nielekeze wale 9,800 walimu na 6,876 wa kada za afya wahakikishe wanaripoti kwa waajiri wao kabla au ifikapo Julai 11, mwaka huu. Mwajiriwa yeyote ambaye hataripoti kwa wakati nafasi yake itachukuliwa na mwingine.

Ofisi ya Rais TAMISEMI haitambadilishia kituo mwajiriwa yeyote mpya kwa kuwa vituo walivyopangiwa ndivyo vyenye uhitaji kwa sasa," alisema.

**KIBANO WAKURUGENZI**

Bashungwa alisema hatosita kumchukulia hatua Mkurugenzi wa Halmashauri atakayechukua kifungu cha fedha cha Kitengo cha Mawasiliano Serikalini.

Alisema katika bajeti ya serikali ya mwaka huu 2022/23, kitengo hicho kitakuwa kipya na kitakuwa na kifungu chake cha fedha ambapo lengo ni kuleta ufanisi katika kutoa taarifa kwa umma.

"Nimeongeza kigezo cha saba kwenye kupima wakurugenzi, kitakuwa ni kuangalia uwajibikaji wa kitengo cha mawasiliano ambapo taarifa itatolewa kila robo mwaka,"alisema.

Aliongeza: "Ninataka kuona kila kitengo cha mawasiliano kwenye mikoa na halmashauri wana vifaa na jambo hili ni maalum, wakurugenzi tafuteni bajeti maalum ya kutekeleza hili, ndio maana nimeweka kigezo hiki."

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan aliagiza kitengo hicho kuwa na kifungu maalum ili kuongeza ufanisi na Maofisa hao kutimiza wajibu wao.

"Rais amewapenda amewaamini, aliniita akasema katika bajeti inayoandaliwa kiwepo na kifungu cha Kitengo cha Mawasiliano serikali na atakayetempa na hiki kifungu namfyatua, nataka mfanye kazi kwa kutimiza majukumu yenu mkiwa na vitendea kazi," alisema.

Alisema kuwa kwa wale watakaoshindwa kutimiza wajibu wao, wasimlaumu kwa kuwa wamepewa miongozo.

Pia aliwataka maofisa hao kuisemea serikali na kukemea upotoshaji unaofanyika.

Katika hatua nyingine, Waziri Bashungwa aliagiza kupewa taarifa kwanini mikoa 15 haijatekeleza maagizo ya kuhuwisha tovuti zao yaliyotolewa na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, katika kikao kilichofanyika Tanga.

"Tulikubaliana tovuti za serikali na akaunti za mitandao ya kijamii lazima zihuwishwe, sasa ninataka kujua hawa 15 hawajafanya kazi hii, ninatoa wiki moja kwa yeyote ambaye hajatekeleza maagizo afanye hivyo," aliagiza.

Alisema Halmashauri 118, mikoa miwili bado hazina Maofisa Habari na kuagiza kufanyika msawazo wa Maofisa Habari na kama kuna eneo wapo wawili na eneo lingine hakuna ifanyike tathmini na msawazo ndani ya mwezi huu.

**KIDATO CHA TANO**

Aliwataka wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha tano mwaka huu kuhakikisha ifikapo Julai 4, mwaka huu wawe wameripoti, vinginevyo nafasi zao watapangiwa wanafunzi wa akiba.

"Walipewa siku 14 za kuripoti shuleni hadi Juni 30, mwaka huu wale ambao hawajaripoti wafanye hivyo hadi Julai 4, mwaka huu, vinginevyo nafasi zao watapangiwa wanafunzi wa akiba na nitoe wito kwa wazazi na walezi nchini kuzingatia hili," alisema.

**MICHANGO SHULENI**

Waziri Bashungwa pia aliagiza Wakuu wa Shule na Walimu Wakuu wasitoze wanafunzi michango yoyote ambayo haijabainishwa kwenye mwongozo na nyaraka za maelekezo ya serikali.

"Wakuu wa shule sekondari lazima washirikishe bodi za shule na kwa shule za msingi lazima washirikishe kamati za shule kupitia miongozo ya serikali na wasitoze michango kinyume cha miongozo ya serikali.

"Mkuu wa shule yeyote ambaye hatazingatia miongozo hii atachukuliwa hatua, Maofisa Elimu wa Wilaya na Mikoa wasimamie hili, wakuu wa mikoa na wilaya simamieni hili ili kuondoa kero na sintofahamu inayojitokeza kwa wakuu wa shule kutozingatia miongozo," alisema.

**TAASISI ZIJITAFAKARI**

Wakati huo huo, Bashungwa pia aliitaka Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, Taasisi ya Soko la Kariakoo na Shirika la Elimu Kibaha kujitafakari kiutendaji.

Kaimu Katibu Mkuu TAMISEMI, Dk. Charles Msonde, alisema moja ya vikwazo wanavyokabiliana navyo maofisa hao ni kutowatumia kuingia kwenye kikao cha kisheria na wamekuwa wakitekeleza majukumu mengine ambayo si yao.

Awali, Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alisema kupitia mkutano wao uliofanyika Tanga, walikubaliana mambo mbalimbali ikiwamo kuongeza ufanisi kwenye utendaji na kutangaza ajenda za kitaifa na taarifa zipelekwe Idara ya Habari Maelezo lakini hakuna kilichofanyika hadi sasa.

# Mwinyi akasirishwa upotoshaji dhidi yake

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema licha ya upotoshwaji wa taarifa kutoka kwa baadhi ya watu kuhusu serikali yake, kamwe hatorudi nyuma katika kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar.

Alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na waandishi wa habari Ikulu Zanzibar na kutoa ufafanuzi wa hoja saba kuhusu kasumba na upotoshaji wa taarifa zinazosambaa katika mitandao ya kijamii.

Alisema kuna taarifa za upotoshajwi kuhusu ukodishwaji wa visiwa 10 vilivyokodishwa na serikali yake na kusisitiza kuwa serikali ya awamu ya nane siyo iliyoanza ukodishwaji wa visiwa.

Alisema siyo jambo geni wala la aibu kukodishwa visiwa hivyo ambapo baadhi ya visiwa vilikodishwa miaka 30 iliyopita.

Dk. Mwinyi alisema kuwa visiwa 10 vilivyokodishwa na serikali yake, vitakuza sekta ya utalii na serikali kupata mapato ambapo zaidi ya dola milioni 440 zitapatikana kwa ukodishwaji wa visiwa hivyo.

"Serikali ina dhamira njema ya kuleta maendeleo na ndio maana tumewekeza katika kuvikodisha visiwa vidogo 52 vilivyopo Zanzibar na hadi sasa tumeshakodisha visiwa 10 na wala visiwa havijauzwa kama baadhi ya watu wanaosambaza taarifa za uzushi katika mitandao ya kijamii," alisema.

Rais Dk. Mwinyi alisema uwekezaji mdogo uliokuwa ukifanywa katika visiwa hivyo hausaidii nchi kwa sababu kodi inayopatikana ni ndogo na watalii wachache kufika huko.

Alisema miaka ya nyuma serikali ilikuwa ikikodisha visiwa kwa Dola 1,000 kwa mwaka, jambo ambalo haliipatii pato serikali na uwekezaji wa sasa ni mkubwa, akitolea mfano kisiwa kimoja cha Kwale kimekodishwa kwa dola milioni 80 kwa mwaka.

Alisema kuwa hakukuwa na usiri katika ukodishwaji wa visiwa hivyo na zabuni ilitangazwa na taratibu zikafuatwa hadi kuwapata wawekezaji waliokodi visiwa hivyo.

Dk. Mwinyi alisema pia kuna upotoshwaji wa taarifa kuhusu Mji Mkongwe wa Zanzibar ambao ni urithi wa wazanzibari ambapo serikali yake inafanya maboresho ya majengo ya mji huo ili urithi wake usipotee.

Alisema pia kuna upotoshwaji wa taarifa kuhusu miradi mbalimbali ya maendeleo inayojengwa ikiwamo masoko, viwanja vya michezo vya kisasa ambayo serikali imeingia ubia na sekta binafsi katika kujenga miradi hiyo.

Rais Mwinyi alisema baada ya serikali kuingia makubaliano na kampuni ya kimataifa ya Dnata kuendeshwa uwanja wa ndege kisasa, yamekuwapo maneno mengi ya upotoshaji.

Alisema Zanzibar inategemea utalii na utalii unaanzia kwenye uwanja wa ndege, hivyo zinahitajika kampuni kubwa zenye kutoa huduma za kisasa.

"Yote wanayosema na waseme maana ni uzushi mtupu lakini sirudi nyuma hata hatua moja, ukweli ndio huu kwamba nina nia njema na wananchi wa Zanzibar na ndio maana ninafanya maendeleo," alisema. Akizungumzia demokrasia, Dk. Mwinyi alisema demokrasia ya CCM ni nzuri na haitoi nafasi ya uongozi kwa uenyeji bali inafuata katiba, kanuni na maadili.

Kuhusu kauli iliyotolewa na aliyekuwa mwasiasa mkongwe Zanzibar, Baraka Shamte, kwamba akimaliza muda wake wa miaka mitano apishe wengine, alisema wananchi ndio watakaompima kutokana na utendaji wake.

Alipoulizwa kuhusu suala la kumsamehe Shamte kutokana na matashi yake kama ambavyo aliomba radhi mwenyewe kupitia mitandao ya kijamii, Dk. Mwinyi alisema msamaha huo haujazingatia taratibu za kumwomba msamaha.

"Baraka amejikita zaidi kuomba radhi kwa chama chake cha CCM kuwa arejeshwe CCM na wala hajaniomba radhi mimi binafsi kutokana na alivyonikashifu," alisisitiza Dk. Mwinyi.

## HABARI KITAIFA



Mwalimu wa fani ya ufugaji wa wanyama kutoka VETA Singida, Hamisi Msangi (kulia), akitoa maelezo kwa mwananchi, kuhusu namna ya ubunifu kwa ajili ya kuongeza tija kwenye kilimo na ufugaji, katika maonyesho ya 46 ya biashara ya kimataifa ya Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wajifungulia getini, watumishi zahanati wasimamishwa kazi

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

WATUMISHI watatu wa Zahanati ya Kashai iliyoko Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera, Reticia Muganyizi (45), Binkwaya Haruna (42) na Linus Balie (32) wamesimamishwa kazi baada ya kinamama wawili waliokuwa wajawazito, kujifungulia katika geti la zahanati hiyo usiku wa kuamkia juzi.

Kinamama hao walifikia uamuzi huo baada ya kufika kwenye zahanati hiyo wakihitaji huduma na wauguzi waliokuwa zamu walikataa kuwafungulia.

Agizo la kusisimamishwa kazi kwa watumishi hao lilitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Moses Machali, baada ya kupata taarifa kutoka kwa Mwenyekiti wa Mtaa wa Kashai Halisi majira ya saa 10:12 alfajiri kuwa kuna mama amejifungulia katika geti la zahanati hiyo baada ya kufika na kubisha hodi na wauguzi wakagoma kufungua.

"Mwenyekiti alinipigia simu akasema kuna mama anajifungulia getini, hakuna mlinzi na wamegonga mlango ili wauguzi wafungue lakini hawafungui, alisema aliamua kuzunguka nyuma ya fensi akiwa na kijana mmoja, akamwomba apande fensi na kuingia ndani, kijana huyo alifanya hivyo na kwenda kuwaita wauguzi hao katika wodi walimokuwa wamelala lakini wakakataa kufungua," alisema Machali.

"Askari walipatikana haraka na saa 10:38 nilikuwa tayari nimefika zahanati ya Kashai, nilishuhudia mwenyewe kwa macho yangu mwanamke mmoja aitwaye Asnath Adamu (33) akijifungulia pale nje ya geti, huku aliyetangulia kujifungua Agnes Malisery (26) nilikuta diwani wa kata Kashai amekwishamwondoa na kumpeleka Kituo cha Afya Zamzam ili apatiwe huduma," alisema.

Alisimulia kuwa akiwa na askari, waligonga mlango na kuita kwa sauti za juu ili wauguzi wafungue mlango waingie lakini hawakufungua na kuwa tukio hilo limemsikitisha, akibainisha kuwapo malalamiko ya wananchi kuwa wamekuwa hawapati huduma usiku.

"Ninazo taarifa nyingi ofisini kwangu kutoka kwa wananchi wakidai kukosa huduma usiku katika baadhi ya vituo vya afya na zahanati katika wilaya yangu, nilichokuwa nahitaji ni kupata ushahidi na sasa nimeupata baada ya kupata taarifa na kufika mwenyewe eneo la tukio na kumshuhudia mmoja akijifungua," alisema.

Kufuatia tukio hilo, mkuu wa wilaya huyo alimwagiza Mkurugenzi wa Manispaa ya Bukoba na wasaidizi wake kuwasimamisha kazi wafanyakazi hao waliokuwa zamu na hatua za haraka za kinidhamu zichukuliwe dhidi yao na yeye apate taarifa ya utekelezaji wa maelekezo hayo kabla ya Julai 6 mwaka huu.

Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Ahmed Njovu, alikiri kupokea maelekeo hayo ya mkuu wa wilaya na kwamba utekelezaji wake unaendelea kwa kuwa kitendo walichokifanya wamekiuka taratibu na kiapo cha kazi na hawafai kuendelea kuwa watumishi wao.

"Tumewasimamisha kazi lakini pia tutawapeleka katika baraza lao la wauguzi ili waone hatua za kuchukua, pia hatua zingine tutapita katika vituo vyote vya afya na zahanati ili kubaini watumishi ambao wamekaa muda mrefu katika vituo vyao vya kazi ili wahamishwe, lengo ni kupuguza tatizo la kuzoea na kushindwa kuwajibika," alisema.

Diwani wa Kashai lilikotokea tukio hilo, Ramadhan Kambuga, alimshukuru mkuu wa wilaya kwa kufika haraka eneo la tukio na kuchukua hatua.

Pia aliwashukuru waendesha pikipiki ambao walitoa msaada mkubwa kwa kinamama hao usiku na kuhakikisha wanajifungua salama.

"Nitakwenda kuzungumza na wananchi wangu wa kata Kashai watulie wasiwe na taharuki, tatizo lililotokea linafanyiwa kazi ili kuhakikisha halijitokezi tena," alisema Kambuga.

Mmoja wa kinamama waliojifungulia katika geti hilo la zahanati, Agnes Malisery (26), mkazi wa Kashai, alisema alipata uchungu saa tisa usiku na kwenda kuwataarifa majirani zake ambao walimtafuta bodaboda ampeleke katika zahanati hiyo huku wao wakimfuata wakitembea kwa miguu na kwamba alipofika, bodaboda aligonga geti bila mafanikio.

"Tulikuta geti limefungwa kwa ndani kwa kufuli, tukaita hakuna anayeitika wala geti halifunguliwi, mpaka wale majirani waliokuwa wakinifuata wakafika, wakaanza kuita na kugonga geti kwa nguvu lakini hatukufanikiwa, ghafla chupa ilipasuka nikaomba wanitandikie kitenge, wakatandika na kuniwekea mpira nikalala," alisimulia.

Alisema kuwa kutokana na kelele zilizokuwapo eneo hilo, watu walizidi kukusanyika na pikipiki akasema anamfuata bibi mmoja aitwaye Doka eneo la Katatorwansi ambaye alimwamsha usiku huo na kufanikiwa kuja naye na kwamba ndiye aliyemsaidia akajifungua.

"Baada ya kujifungua, bahati nzuri tulikuwa na wembe bibi huyo akawa anatafuta uzi wa kukata kufunga kitovu cha mtoto akakosa, akakata kipande cha kanga na kufunga kitovu, lakini wakati huo Diwani wa Kata ya Kashai alikuwa amefika akanipakiza katika gari lake na kunipeleka Kituo cha Afya Zamzam," alisema.

Naye Asanath Adam (33), mkazi wa Rwome, Kata Kashai ambaye pia alijifungulia nje ya geti la zahanati hiyo siku hiyo, alisema alipata uchungu saa 9:30 usiku na kufika katika zahanati hiyo akiwa na bodaboda saa 10:25 na kukuta watu wengi na kuanza kushangaa.

"Kumbe watu hao walikuwa wakimshuhudia mwenzangu aliyetangulia kujifungua hapo getini, baada ya kufika nikashuka kutoka katika bodaboda, nikamkuta diwani wa Kashai akimpakiza mwenzangu ampeleke kituo cha afya Zamzam akaniambia nami niingie kwenye gari lake anipeleke huko, nikamwambia siwezi tena kupanda gari maana mtoto amekwishaanza kutoka," alisema.

Alisema naye akiwa na wananchi wengine walijaribu kugonga geti na kuita kwa sauti kubwa bila mafanikio, akaomba wamtandikie kitenge chini wakamtandikia, akalala na kujifungua kwa kusaidiwa na huyo bibi aliyemkuta eneo hilo akimsaidia mwenzake, huku wananchi wakishuhudia.

"Baada ya kujifungua na mimi nikaletwa hapa Zamzam na mtoto wangu, tunaendelea vizuri, tunawashukuru wote waliotoa msaada kwetu maana bila wao sijui kama tungekuwa wazima au hatujui kama watoto wetu wangekuwa wazima," alisema mama huyo.

Mmoja wa watu walioshuhudia wanawake hao wakijifungua nje ya geti la zahanati hiyo, Masoud Shaban, mkazi wa Kashai, alisema baada ya kusikia kelele, yeye na jirani yake walifika eneo la tukio na kumkuta mwanamke mmoja akiendelea kupatiwa huduma na bibi mmoja na wao kuombwa msaada wa maji.

"Tulikimbia kutafuta maji na wembe kwa ajili ya kumsafishia mama huyo tukayaleta akasafishwa lakini muda mfupi aliletwa mwanamke mwingine akiwa na hitaji hilo hilo la kutaka kujifungua naye alijifungulia nje ya geti maana mlango wa zahanati haukufunguliwa kabisa," alisema Shaban.

Kufuatia tukio hilo, polisi walifika katika zahanati hiyo walifanikiwa kuingia ndani ya zahanati kwa maelekezo ya mkuu wa wilaya na kuwatoa watumishi hao na kuondoka nao.

## Polisi wadaiwa kukataa kufanya uchunguzi

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

ASKARI wa Kituo cha Polisi Misigiri katika Wilaya ya Iramba mkoani Singida wanadaiwa kukataa kufanya uchunguzi wa tukio la Stella Jingu (38) aliyepotea katika mazingira ya kutatanisha miaka miwili iliyopita wakitaka kwanza wapewe fedha na ndugu wa mwanamke huyo.

Inadaiwa askari hao (majina tunayahifadhi) walitaka wapewe 45,000 ndipo waweze kufuatilia suala hilo kwenye mtandao lakini ndugu waliposhindwa kutoa fedha hizo kutokana na hali ngumu ya maisha waliyonayo, wakasema na wao hawawezi kufuatilia tukio hilo.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Binilith Mahenge, alielezwa hayo na mtoto wa mwanamke huyo aliyepotea, Roda Philipo wakati wa mkutano wa hadhara wa kusikiliza kero za wananchi uliofanyika Kijiji cha Misigiri wilayani Iramba.

Roda alisema mama yake alipotea katika mazingira ya kutatanisha tangu Februari 2020 ambapo siku ya tukio, mlango wa nyumba aliyokuwa akiishi ulikutwa upo wazi huku nguo na vitu mbalimbali vilivyokuwamo ndani vikiwa vimetupwa ovyo.

Alisema kuwa baada ya tukio hilo, kaka wa mwanamke aliyepotea aitwaye Nyerere Jingu na shangazi yake Mama Zahara, walikwenda kutoa taarifa katika Kituo cha Polisi Misigiri lakini katika hali ya kushangaza askari waliokuwapo zamu, walisema hawawezi kufuatilia suala hilo hadi wapewe pesa.

Roda alisema baada ya kugonga mwamba polisi, walikwenda kutoa taarifa kwa viongozi wa serikali ya Kijiji cha Misigiri ambapo Mwenyekiti wa Kijiji, aliitisha mkutano wa kijiji kuwaomba wananchi kama kuna mtu alikuwa anamdai Stella Jingu (aliyepotea) ajitokeze alipwe ili amrudishe alikompeleka.

Hata hivyo, hakuna mtu yeyote aliyejitokeza na hadi sasa wamekuwa wakifuatilia wenyewe kwa ndugu wengine waliopo nje ya wilaya na vijiji jirani bila mafanikio huku Jeshi la Polisi likituhumiwa kutofuatilia tukio hilo.

"Mama yangu alipotea tangu 2020 na hajulikani aliko hadi sasa, tukienda polisi wanasema tutoe fedha ndipo watafuatilia suala hili, lakini hali yetu kiuchumi ni mbaya. Tumeshindwa kupata fedha zinazohitajika, tunakuomba Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa utusaidie, hatujui kama mama yetu yupo hai au alishakufa," alisema.

Kufuatia malalamiko hayo, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mahenge, alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Iramba na Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa, Lucas Mwakatundu, kufuatilia suala hilo na apewe ripoti ndani ya wiki mbili.

"Kama kweli polisi hawakulifanyia kazi tukio hili kwa kutaka kwanza wapewe pesa, itabidi hatua zichukuliwe kwa wahusika, pia muangalie kama walisajili tukio hilo hapo kituoni," aliagiza.

# Onyo latolewa kwa majangili

**Na Elizabeth Zaya**

KATIBU Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Profesa Eliamani Sedoyeka, ametuma salamu kwa wale wote watakaothubutu kujihusisha na ujangili wa wanyamapori, kwamba watakiona cha moto.

Prof. Sedoyeka alitoa kauli hiyo jana Dar es Salaam wakati akikabidhiwa magari 10 kutoka Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP).

"Kama kuna mtu anawaza kufanya ujangili, ajue kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii tumejipanga na hatapata nafasi ya kufanya hivyo akabaki salama kwa sababu tumejipanga," alionya.

Prof. Sedoyeka alisema kwa sasa idadi ya wanyamapori imeongezeka katika maeneo mengi, hivyo wamejipanga kuhakikisha maliasili hiyo inalindwa kwa nguvu zote na kwamba yeyote atakajaribu kuichezea, hatua kali zitachukuliwa dhidi yake.

"Nchi yetu ipo katika mapambano makali dhidi ya ujangili na kulinda rasilimali za nchi hii, na sisi kama wizara tutahakikisha tunazilinda ili ziendelee kutumika vizuri katika Taifa na kubaki kwa ajili ya vizazi vijavyo," alisema.

Pia alisema magari hayo 10 ambayo wamepokea kutoka UNDP, yatasaidia kuongeza nguvu kwa serikali katika jitihada za kupambana na ujangili wa wanyamapori.

Mwakilishi Mkazi UNDP, Christine Musisi, alisema Wizara ya Maliasili na Utalii wamekuwa wakishirikiana kwa muda mrefu na watahakikisha wanaendeleza ushirikiano huo.

Pia alisema sekta ya utalii ni miongoni mwa zinazochangia kwa kiwango kikubwa uchumi wa nchi, hivyo wataendelea kuisaidia ili kuwezesha kufanya kazi zake vizuri.

# Miaka 60 Uhuru wa Burundi na ndoto za kuwa shirikisho

**Na Moshi Lusonzo**

JUZI Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alimwakilisha Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan katika sherehe za Maadhimisho ya Miaka 60 ya Uhuru wa Jamhuri ya Burundi.

Akiwa huko, Dk. Mwinyi alisema Serikali ya Tanzania inaridhishwa na uhusiano mzuri uliopo kati ya Serikali ya Tanzania na Burundi.

Alisema kuwa kabla ya enzi za ukoloni, watu wa nchi hizo mbili hawakujua mipaka kwa kuwa walishirikiana kwa uhuru mara kwa mara kupitia biashara na shughuli zingine za kijamii na kitamaduni.

Dk. Mwinyi alisema kuwa hata baada ya kuwekwa mipaka, bado wananchi wa nchi mbili hizo wameendelea kuwa wamoja na kushirikiana.

**NDOTO ZA SHIRIKISHO**

Historia inaeleza kuwa mwaka mmoja kabla ya siku ya uhuru wa nchi hiyo kulikuwa na uchaguzi wa kwanza chini ya usimamizi wa Umoja wa Mataifa (UN) na chama kilichoshinda katika uchaguzi huo (UPRONA), kilichoongozwa na Mfalme Lous Rwagasore, kiliunganisha pande mbili kwa maana ya Watusi na Wahutu.

Hata hivyo, Jumamosi ya Oktoba 13, 1962, Rwagasore, ambaye alifikiriwa anajenga uelewano wa kuishi pamoja kati ya pande hizo, aliuawa.

Kifo chake kilikatisha ndoto ya shirikisho la Tanganyika na Burundi, alilokuwa analifikiria Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Baada ya Uhuru wa Tanganyika, katika hotuba yake kwenye mkutano wa TANU mwaka 1962, Mwalimu Nyerere alionyesha wazi kukerwa na mauaji dhidi ya Rwagasore.

Ikumbukwe kuwa eneo lote la Tanganyika, Rwanda na Burundi kipindi hicho lilijulikana kama Afrika Mashariki la Kijerumani (GEA). Hata hivyo, GEA iligawanywa kati ya Uingerezam, Ubelgiji na Ureno kuwa mamlaka ya Shirikisho la Kimataifa.

Historia inaeleza kuwa Rwagasore aliungana na Nyerere kutetea uhuru, Uafrika na ujamaa na kuwatia wasiwasi wakoloni.

Kwa mujibu wa mchambuzi wa Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC), Ezekiel Kamwaga, safari ya mwisho ya Rwagasore kutembelea Tanganyika ilikuwa miaka ya 1960 alipomsimulia Mwalimu Nyerere ndoto yake moja kubwa - kwamba baada ya nchi zao kupata uhuru, waunde Shirikisho la Tanganyika na Burundi.

"Hiyo ndiyo kumbukumbu iliyobaki kichwani kwa Mwalimu wakati rafiki yake huyo akipanda ndege kurejea Bujumbura," anasema Kamwaga, aliyewahi kuwa Ofisa Habari wa Klabu ya Simba na jijini Dar es Salaam.

Hata hivyo, Rwagasore aliuawa kwa kupigwa risasi baada ya kuwa waziri mkuu kwa wiki mbili tu na kifo chake kuonekana kama kuzima ndoto za shirikisho hilo.

Mwanahabari na mchambuzi Kamwaga alikaririwa wiki hii akibainisha kuwa sasa kuna mambo yanaonekana kwenye korido viongozi wa nchi hizo kutaka kurejea ndoto za waasisi wa mataifa yao.




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi na mkewe Mariam Mwinyi, wakiwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume Zanzibar juzi, wakitokea nchini Burundi, kumuwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika sherehe za maadhimisho ya miaka 60 ya nchi hiyo. **PICHA: IKULU**

# Samia aipongeza Muhimbili kutenganisha watoto pacha

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan amewapongeza madaktari na wauguzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kwa kufanikisha upasuaji wa kuwatenganisha watoto pacha walioungana.

Jopo la wataalam wa afya 31 wa ndani na nje ya nchi juzi lilifanya operesheni hiyo iliyochukua saa saba hadi kukamilika kwake na hatimaye Neema na Rehema kila mmoja anaishi kwa kujitegemea.

Katika ukurasa wake wa Twiter jana, Rais Samia aliandika ujumbe wa kuipongeza timu hiyo, akisema: "Ninawapongeza madaktari na wauguzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa kufanikisha upasuaji wa kuwatenganisha watoto pacha walioungana.

"Hii ni hatua muhimu katika kuboresha matibabu ya kibingwa. Ninawaombea watoto Rehema na Neema wapone haraka."

Timu ya wataalamu hao ilianza operesheni majira ya saa tatu asubuhi na kumalizika saa tisa alasiri. Upasuaji huo ulihusisha kutenganisha ini, mishipa mikubwa iliyomo humo pamoja na kuitenganisha ngozi iliyopo kwenye moyo.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi jioni mara baada ya kufanikisha kuwatenganisha, Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Watoto wa Muhimbili, Zaitun Bokhary, alisema ugumu ulikuwa ni katika kutenganisha ini.

"Watoto hawa walikuwa ini lao limeungana kabisa na kuwa kama kitu kimoja na kuna baadhi ya mishipa mikubwa katika ini ilikuwa imeungana kwa hiyo ilikuwa ngumu kutenganisha ini," alisema.

Watoto hao walizaliwa Septemba 21, 2021 kwa njia ya upasuaji wakiwa na kilo 4.9 wote kwa pamoja katika Hospitali ya Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu ambapo walipewa rufani kwenda Hospitali ya Kanda ya Ziwa (Bugando) na baadaye Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Upasuaji kama huo ni mara ya tatu kufanyika nchini. Wa kwanza ulifanyika mwaka 1994 ukihusisha watoto wawili wa kiume waliokuwa wameungana kwenye tumbo.

"Upasuaji wa pili ulifanyika mwaka 2018 ukihusisha watoto wawili wa kiume wanaoishi Kisarawe ambao wana miaka mitatu na miezi tisa sasa na wanaendelea vizuri," alisema Dk. Zaitun

# Mtanzania apewa tuzo na Ufaransa

**Na Faustine Feliciane**

SERIKALI ya Ufaransa imemtunuku tuzo ya heshima Mtanzania Dk. Mwatima Juma kwa juhudi na kujitolea katika kuendeleza kilimo hai Tanzania.

Tuzo hiyo kubwa imetolewa na Waziri wa Masuala ya Kilimo wa Ufaransa, Julien Denormandie, ambapo Dk. Mwatima alikabidhiwa jijini Dar es Salaam na Balozi wa Ufaransa nchini, Nabil Hajlaoui.

Akizungumza wakati wa hafla fupi ya kukabidhi tuzo hiyo, Balozi Hajlaoui alisema tuzo ya heshima hutolewa kwa mtu aliyefanya makubwa kwenye sekta mbalimbali ambapo tuzo hiyo ilishawahi kutokewa kwa mwana wa mfalme wa Uingereza (Prince Charles) na watu wengine mashuhuri.

"Dk. Mwatima Juma ameonyesha namn alivyojipambanua kwenye sulaa zima la kilimo hai, ameonyesba namna gani wanawake wanaweza kuleta mabadiliko makubwa, amekuwa akiendesha harakati za kuhamasisha kilimo endelevu (kilimo kisichotumia kemikali)," alisema Balozi Hajlaoui.

Alisema kama ilivyo kwa Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan alivyoonyesha namna gani wanawake wanaweza kuleta mabadiliko katika nyanja za uongozi, Dk. Mwatima ameonyesba na yeye kwenye sekta ya kilimo namna ambavyo anaweza kuleta mabadiliko chanya kwenye sekta hiyo kwa kuhimiza kilimo endelevu.

Akipokea tuzo hiyo mbele ya familia yake, Dk. Mwatima alisema tuzo hiyo imezidi kumpa moyo wa kuendelea kuhamasisha kilimo endelevu nchini.

"Sikutarajia kupata tuzo hii kubwa ya heshima, hii itanifanya niendele kuhamasisha Watanzania kulima pasipo kutumia kemikali kwa mustakabali wa afya zetu na uhai wa ardhi yetu," alisema Dk. Mwatima.

Alisema Watanzania wanapaswa kuufahamu kilimo cha kutumia kemikali siyo tu kinaua ardhi lakini pia kinafanya mkulima asiwe huru na kilimo.

"Ukianza kutumia kemikali maana yake unaingia kwenye mnyororo wa matumizi kila msimu, hii inapelekea ardhi yetu kufa na kwa maana hiyo huwezi tena kulima bila kutumia hizo kemikili, tunapaswa kurudi kwenye kilimo chetu cha asili.

"Wazee wetu walikuwa wanalima bila kutumia kemikali na hazikuwapo, lakini walikuwa wakipata mazao ya asili na kuepuka na magonjwa mengi yasiyoambukiza kama kisukari, shinikizo la damu na kansa," alisema Dk. Mwatima.

Dk. Mwatima ni mmiliki wa kituo cha kilimo hai cha PPIZ kilichoko Zanzibar na mmiliki wa shamba la asili la Msonge. Pia ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Kuendeleza Kilimo Hai Tanzania (TOAM).




Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Angelina Ngalula, akizungumza wakati wa hafla ya kumpongeza baada ya kuteuliwa kuwa Mwanamke wa kwanza Mwenyekiti wa Baraza la Biashara la Afrika Mashariki (EABC), iliyoandaliwa na TPSF, jijini Dar es Salaam juzi jioni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NEMC yabaini tatizo la kemikali kiwanda sukari

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limefanya ziara ya kushtukiza katika Kiwanda cha Sukari cha Mtibwa na kubaini kemikali zimeteketezwa bila kufuata sheria za usimamizi wa mazingira.

Kufuatia hali hiyo, NEMC imepiga marufuku halmashauri nchini kuingilia shughuli za uteketezaji wa kemikali bila kufuata sheria, hali inayohatarisha usalama wa viumbe hai.

Akizungumza katika ziara hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema wamebaini Ofisa Mazingira wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero aliteketeza kiholela shehena ya kemikali zilizokwisha muda wake za kiwanda hicho bila kufuata sheria.

"Ninachotaka kuweka sawa kwa halmashauri nchi nzima usifanye kuteketeza au kushughulikia kemikali bila kutoa taarifa kwa Mkemia Mkuu wa Serikali na NEMC ambao wao ndiyo wanaotoa vibali na ruhusa za kuteketeza hizo taka hatarishi na taka zozote zile za sumu," alisema.

Aliongeza kuwa anatoa angalizo hilo kwa halmashauri zote zifuate utaratibu huo huku kivitaka viwanda vyote nchini kufuata sheria na kanuni za uteketezaji wa kemikali kwa kuziona mamlaka husika.

"Utupaji holela wa taka za sumu unaleta athari kwa viumbe hai na mazingira kwa ujumla, hivyo hazina budi kuteketezwa, nitoe rai kwa viwanda vyote viwe vya nguo, vya bidhaa zozote kuhakikisha vinapata kibali kwa Mkemia Mkuu wa Serikali na NEMC kabla ya uteketezaji," aliagiza. Alifafanua kuwa kisheria vyombo vinavyotunza kemikali au kemikali zinazoisha muda wake vinapohitajika kutekelezwa taratibu zilizopo ni kupeleka maombi kwa Mkemia Mkuu na NEMC ili kubaini njia na mbinu salama ya kuteketeza kemikali.

Aliitaka Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero kuwasilisha vielelezo rasmi vya uteketezaji wa kemikali hizo ulivyofanyika.

Meneja NEMC Kanda ya Morogoro Rufiji, Amina Kibola, aliwasihi watu wanaofanya shughuli ambazo zinazalisha taka hatarishi ikiwamo kemikali, kimaabara na migodini, kufuata kanuni, sheria na taratibu wakati wa uteketezaji. Meneja wa Udhibiti wa Majanga wa Kiwanda hicho, Moses Tenda, alisema wanapopata taka za sumu au kemikali wamekuwa wakishirikisha uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero ambao hutoa taratibu na kusimamia kuharibu taka hizo. "Wamekuwa wakisimamia utaratibu wa kuziharibu taka hizo tunazozalisha kulingana na taratibu zinavyotaka," alisema meneja huyo.

# Mkuu Majeshi aahidi maboresho SUMAJKT

**Na Romana Mallya**

WAKATI Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Stergomena Tax, akilitaka Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT), kuangalia uwezekano wa kuanzisha mfuko wa kusaidia vijana kupata mitaji, Mkuu mpya wa Majeshi ya Ulinzi Tanzania (JWTZ), Jenerali Jacob Mkunda, amesema ipo kazi ya kulifanya shirika hilo kuwa kubwa.

Walisema juzi kwa nyakati tofauti wakati wa kilele cha maadhimisho ya miaka 41 ya SUMAJKT tangu kuanzishwa kwake mwaka 1981 yaliyokwenda sambamba na uzinduzi wa kitabu cha shirika hilo.

Kitabu hicho kimeelezea chimbuko la SUMAJKT, miradi inayotekelezwa, mafanikio yake na mipango mbalimbali ya baadae iliyonayo.

Waziri wa Ulinzi, Tax, alisema kama inawezekana SUMAJKT wanaweza kuanzisha mfuko wao wenyewe utakaowezesha vijana kupata mitaji na kuweza kufanya shughuli mbalimbali.

"Ni vijana ambao tumewalea wenyewe bila shaka tunawaamini tunaweza kuweka utaratibu kuona mfuko huo unavyoweza kufanya kazi. Ni vitu vinavyohitaji kufikiria na kuona vinaweza kufanyiwa kazi kwa namna gani," alisema.

Waziri Tax alisema wakati shirika likianzishwa lilikuwa na vitengo tisa na miradi 25 ambayo ilikuwa inatekelezwa katika vikosi 19 ambapo hadi sasa lina kampuni 24 na shule mbili na zaidi ya miradi 221 katika sekta za ujenzi, kilimo, mifugo, viwanda, biashara na huduma.

Alisema shirika limeweza kutoa gawio kwenda mfuko mkuu wa serikali ambapo katika mwaka wa fedha 2017/18 na 2021/22, jumla ya Sh. bilioni 4.666 zimetolewa.

Waziri huyo alisema mchango wao katika ajira umeendelea kuongezeka hadi 16,000 mwaka 2021 na zikijumlishwa na zisizo rasmi ni zaidi ya hapo.

Alisema miradi ya kimakakati ya uvuvi na mbegu bora itachangia kwa kiasi kikubwa katika usalama wa chakula.

Alisema kutokana na changamoto za ulimwengu, nchi inakabiliwa na uhaba wa baadhi ya bidhaa ikiwamo mafuta ya kula.

"Pamoja na kwamba hii ni changamoto, naomba tuitumie kama fursa ya moja ya maeneo ya uzalishaji wa kimkakati, tunao uwezo tuutumie kwa kuzalisha mazao kama alizeti, tutoe uzito zaidi tuwe sehemu ya kilimo cha mkakati na kuisaidia serikali kuziba pengo la mafuta ya kula lilipo," alisema.

Mkuu wa Majeshi Nchini, Jenerali Mkunda, alisema lengo la kuanzishwa kwa shirika hilo ambalo linasherehekea miaka 41, ni uzalishaji mali kwa faida na hivyo kuipunguzia serikali gharama ya malezi ya vijana wanaojiunga na mafunzo ya JKT.

"Kwa kutumia vyanzo vyake vya ndani ya shirika limeendelea na shughuli za uzalishaji mali kupitia kampuni zake tangu na viwanda, pamoja na kuipunguzia serikali gharama, shirika limekuwa likichangia pato la taifa na kodi mbalimbali zinazotokana na bidhaa na huduma inazozizalisha," alisema. Pia alisema limekuwa mafunzo kwa vitendo kwa vijana wanaojifunza stadi mbalimbali za kazi wanapomaliza.

"Mara nyingi tumeaminiwa na kupewa miradi mikubwa kwa sababu ninyi (wizara) mmekuwa mnatusemea vizuri na kuiaminisha serikali kwamba tunaweza, na kweli tunaweza," alisema.

Aliongeza: "Pamoja na mafanikio, bado tunayo kazi ya kulifanya shirika kuwa kubwa lenye sifa kibiashara litakalokuwa na uwezo wa kuliwezesha Jeshi la Kujenga Taifa kuendesha shughuli zake lenyewe," alisema.

Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Meja Jenerali Rajabu Mabele na Ofisa Mtendaji Mkuu wa SUMAJKT, alisema shirika linaendelea kutekeleza mkakati wake wenye lengo la kuongeza mapato na faida kiuchumi na kijamii kwa kuboresha viwanda, kilimo, ujenzi na miradi ya kibiashara iliyopo na kuanzisha mipya.

Pia alitumia fursa hiyo kuwashukuru wale wote waliowahi kuliongoza shirika hilo tangu kuanzishwa kwake ambao wametoa mchango wao ambao sasa wanasherehekea miaka 41.

Mwenyekiti wa Bodi ya SUMAJKT, Meja Jenerali (mstaafu) Farah Mohamed, alisema bodi hiyo itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuhakikisha inatumia gharama ndogo kutegemea maelekezo itakayopewa.

Akizungumza kwa niaba ya Wakuu wa Mikoa, Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Meja Jenerali Charles Mbuge, aliwapongeza Mkuu wa Majeshi Jenerali Mkunda na Mnadhimu Mkuu wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Luteni Jenerali Salum Haji Othman kwa kuaminika na Rais Samia Suluhu Hassan kuteuliwa katika nafasi walizokabidhiwa.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hoja za CAG zifanyiwe kazi kunusuru uhai wanyamapori

**KATIKA** tafsiri ya nguzo kuu za uchumi wa Tanzania, utalii una nafasi kubwa kihistoria. Kwa mujibu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, sekta hii kwa sasa inachangia robo ya fedha za kigeni zinazoingia nchini na asilimia 17.5 ya Pato la Taifa.

Kadri mtu anavyozama kuichambua sekta ya utalii na maliasili, anabaini kuna makundi makuu ya wanyamapori ambao ndiyo vivutio vinavyowafaya wageni kusafiri kutoka mbali kuja kuwashuhudia hapa nchini.

Ikirejewa Sera ya Wanyamapori ya Tanzania (2007) inabainisha kuwa historia ya uhifadhi wa wanyamapori nchini ilianzia mwaka 1891. Kwa lugha rahisi, ni miaka 131 iliyopita.

Hiyo ilikuja kama matokeo ya kuzaliwa kwa sheria za kudhibiti uwindaji zilizoanzishwa na utawala wa Kijerumani uliokuwapo katika zama hizo.

Hifadhi ya kwanza ya wanyamapori nchini ilianzishwa na Wajerumani hao miaka 14 baada ya kutunga sheria katika ukanda wa hifadhi maarufu ya sasa iitwayo Pori la Akiba Selous, mwaka 1905.

Baada ya kupita miaka 16 ya hifadhi kuanzishwa, Tanganyika ikiwa chini ya utawala wa mkoloni mpya, Uingereza, mwaka 1921, kukaanzisha Idara ya Wanyamapori sambamba na mwaka mmoja baadaye, serikali ilitangaza rasmi Pori la Akiba Selous.

Sera inafafanua kuwapo historia ya ushuhuda wa hifadhi nyingine mbili kuanzishwa miaka sita baada ya hatua ya mwisho mwaka 1922. Hapo panatajwa iliyokuwa Bonde Kuu Funge la Ngorongoro (sasa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro) na Pori la Akiba Serengeti (sasa Hifadhi ya Taifa Serengeti).

Wakati wanyamapori wakiwa na mchango mkubwa katika uchumi lipo tatizo la madhila ya kuuawa kwa kugongwa na magari Tanzania, yanayotumia barabara kubwa zinazopita katika hifadhi za taifa.

Miaka mitatu iliyopita, Wizara ya Maliasili na Utalii, iliwasilisha taarifa bungeni kuhusu dosari ya vifo vya wanyamapori vinavyotokana na ajali za magari katika hifadhi.

Takwimu hizo zilibainisha kwamba, mwaka 2014 wanyamapori waliogongwa walikuwa 351; mwaka 2015 (361); na mwaka 2016 walikuwa 218. Hii, ni dosari ambayo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) aliinyooshea kidole kwenye ripoti yake ya ukaguzi ya mwaka 2018/19, akiwa na takwimu za kitaalamu zinazoonesha namna sekta hiyo inavyohujumiwa.

Huku kukiwa na angalizo hilo la kitaalamu kutoka kwa CAG miaka iliyopita, ripoti mpya ya mdhibiti huyo kwa 2020/21 inaonyesha vifo vya wanyapori 614 kutokana na ajali za barabarani katika kipindi cha mwaka mmoja, sawa na wastani wa vifo vya wanyamapori 51 kila mwezi.

Nipashe tunafikiri kuna haja hatua madhubuti za usalama zinapaswa kuchukuliwa kuzuia uzembe wa madereva ndani ya barabara zinazopita kwenye hifadhi za taifa, kwa kuwa pasi na kufanya hivyo, kuna uwezekano wa wanyamapori kuendelea kuuawa kwa ajali za barabarani.

Ni maoni yetu kwamba serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), ipitie upya taratibu za uendeshaji salama wa magari ndani ya hifadhi za taifa nchini ili kudhibiti ajali zinazoua wanyamapori hifadhini.


Nipashe pia tunaishauri mamlaka husika kuimarisha teknolojia ya kufuatilia wanyamapori, tukizingatia hoja ya CAG kwamba hifadhi za taifa zote 22 zinakabiliwa na tatizo la kukosekana kamera za barabarani, hivyo kushindwa kutambua wahusika wanaosababisha ajali hizo.

Vilevile tunashauri serikali itunge sheria ndogo zitakazoongoza utozaji wa faini za kusababisha ajali katika maeneo ya mbuga na kuzisimamia ipasavyo, kwa sasa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) halina sheria ndogo za kutoza faini na adhabu, ambapo tozo au faini hutolewa kulingana na Kanuni za Taifa za Uhifadhi wa Wanyamapori, ambazo hazimfungi mtu katika mahakama za sheria.

Ni katika kuzingatia hali hiyo, tunafikiri kuna haja mamlaka husika zitunge sheria ndogo zitakazoongoza utozaji wa faini za kusababisha ajali katika maeneo ya mbuga na kuzisimamia ipasavyo. Pia, zibuni na kusimamia njia mbalimbali za usalama kama vile kuweka kamera za barabarani, ili kudhibiti ajali na kulinda wanyamapori.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Vyama visivyopata ruzuku vipambane kutafuta fedha

Na Sabato Kasika

**BAADHI** ya vyama vya siasa nchini vimekuwa vikilalamikia ruzuku ya serikali, vikidai kukosa fedha kunasababisha vishindwe kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Malalamiko hayo yamekuwapo kwa muda mrefu baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu wa kwanza ndani ya mfumo wa vyama vya siasa, uliofanyika mwaka 1995 baada ya kurejeshwa mwaka 1992.

Ikumbukwe kuwa dhamira njema ya serikali katika mwaka huo wa uchaguzi, ilitoa ruzuku kwa vyama vyote vya siasa ambavyo vilikuwa na usajili wa kudumu, ili vishiriki kikamilifu kwenye uchaguzi huo.

Lakini baada ya uchaguzi huo, serikali iliondoa ruzuku hiyo kwa baadhi ya vyama kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo matumizi mabaya ya fedha hizo na migogoro ndani ya vyama.

Badala yake iliweka utaratibu wa kisheria wa utoaji wa ruzuku hiyo, baadhi ya kigezo ni vyama kutakiwa kupata kura za ushindi wa angalau asilimia tano ya kura zote pamoja na kuwa na wawakilishi bungeni.

Tangu uchaguzi wa mwaka 2000, ni vyama vichache ambavyo vilianza kupata ruzuku, vikiwamo vya CUF, ACT-Wazalendo, CCM, NCCR-Mageuzi na CHADEMA, lakini baadhi yake navyo vimejikuta vikikosa wawakilishi.

Kwa hali hiyo vinalazimika kutafuta njia nyingine ya kujiendesha, kutokana na kukosa ruzuku kwa kuwa havikidhi vigezo vinavyoelekezwa na kifungu cha 16 cha Sheria ya Vyama vya Siasa Na. 5 ya mwaka 1992.

Sheria hiyo ambayo ilifanyiwa marekebisho inaeleza vigezo vinavyotumika ili chama kipate ruzuku ni kuangalia matokeo ya uchaguzi kuona kama kimepata asilimia 5 ya kura na kushinda nafasi za ubunge ama udiwani.

Kwa mazingira kama hayo kama

**Kwa hali hiyo vinalazimika kutafuta njia nyingine ya kujiendesha, kutokana na kukosa ruzuku kwa kuwa havikidhi vigezo vinavyoelekezwa na kifungu cha 16 cha Sheria ya Vyama vya Siasa Na. 5 ya mwaka 1992.**

chama kimekosa kupata asilimia hiyo, ninadhani ni vyema kipambane kivyake kutafuta njia nyingine ya kupata vyanzo vya mapato badala ya kuomba ruzuku bila vigezo.

Ingependeza kama vyama visivyo na uwakilishi vikajipanga, kwa ajili ya kujenga mtandao wa wanachama, wadau pamoja na mikakati ya kusaka fedha kupitia njia mbalimbali ikiwamo hata kuuza kadi za chama.

Njia nyingine inayoweza kutumika na kujiendesha bila kutegemea ruzuku ya serikali, ni michango ya wanachama, harambee na kuchangiwa na marafiki, kuuza kofia, sare, bendera na vipeperushi.

Lakini pia ni vyema viongozi wa vyama wakatambua kuwa vigezo vilivyowekwa na sheria vinasaidia kuvifanya vyama kuwa makini katika ufanyaji siasa na hatimaye kufikia vigezo vya kuviwezesha kupata ruzuku.

Si vibaya viongozi wa vyama ambavyo havipati ruzuku wakajiuliza, ni njia gani wenzao wamefanikiwa kupata vigezo, ili nao waige mbinu hizo kwa lengo la kuimarisha mitandao mipana ya vyama vyao itakayoviwezesha kujiendesha.

Ni muhimu vyama visivyo na ruzuku kutambua kuwa fedha za umma zina matumizi mengi ikiwamo kuboresha miundombinu ya huduma za jamii kama elimu, afya, maji na nyingine nyingi, hivyo si rahisi kuzipata bila vigezo.

Ruzuku ya vyama vya siasa ni fedha zinazotolewa na serikali kwa vyama vya siasa vilivyokidhi vigezo kama sheria inavyotaka, kwa ajili ya kusaidia shughuli za uendeshaji wa vyama hivyo.

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ndiyo yenye jukumu la kugawa ruzuku ya kila mwezi kwa vyama vya siasa vyenye sifa kwa mujibu wa sheria, hivyo njia rahisi kwa kila chama kupata fedha za kujiendesha ni kubuni miradi.

HABARI KITAIFA



Mfanyabiashara kutoka Burundi, Mariam Ndayisenga, akipanga bidhaa zake katika viwanja vya Maonyesho ya 46 ya biashara ya Kimataifa, Julius Nyerere, Sabasaba barabara ya Kilwa, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# TRA yakusanya Tril. 22/- mwaka mmoja

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imekusanya Sh. trilioni 22.28 kwa mwaka wa fedha 2021/22, yaani katika kipindi cha kati ya Julai 2021 na Juni 2022, sawa na ufanisi wa asilimia 99.22 ya lengo la makusanyo ya Sh. trilioni 22.45. Kiwango hicho ni sawa na ongezeko la Sh. trilioni 4.13 kulinganishwa na kiwango cha makusanyo ya Sh. trilioni 18.15 kilichofikiwa kwa kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2020/21. Ongezeko hilo ni sawa na ukuaji wa makusanyo kwa asilimia 22.77. Kwa mujibu wa taarifa ya TRA iliyotolewa jana, katika robo ya nne ya 2021/22, makusanyo yalikuwa Sh. trilioni 5.59 ilhali lengo lilikuwa Sh. trilioni 5.3, sawa na ufanisi wa asilimia 105.47.

"Ufanisi huu wa kiutendaji ni matokeo ya kuendelea na matumizi ya mifumo ya kieletroniki katika usimamizi na ukusanyaji wa kodi, mazingira ya ufanyaji biashara nchini na mwenendo wa ulipaji kodi kwa hiyari," TRA ilifafanua katika taarifa yake hiyo.

# Dar, Hamburg waingia makubaliano sekta nne

**Na Mary Geofrey**

MAJIJI ya Dar es Salaam na Hamburg la Ujerumani yametia saini mkataba wa ushirikiano katika sekta za elimu, afya, ujasiriamali na sanaa.

Mkataba huo ulitiwa saini juzi jijini Dar es Salaam kati ya Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Omary Kumbilamoto na mwenzake wa Hamburg, Ujerumani, Jinken Bruns.

Akizungumza muda mfupi baada ya kutia saini makubaliano hayo, Kumbilamoto alisema mkataba huo pia una lengo kupendezesha Jiji la Dar es Salaam na kusaidia kuitangaza Tanzania kimataifa na kukuza uchumi.

"Niwapongeze wenzetu wa Jiji la Hamburg kwa upendo wao kwenye kujitoa kusaidia katika sekta mbalimbali hasa ya mazingira baada ya kuahidi kutupatia fedha za kupendezesha mji wetu," alisema Kumbilamoto.

Alisema ujio wa ugeni huo ni matokeo ya kampeni ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuitangaza Tanzania kupitia filamu ya Tanzania The Royal Tour.

Alisema kuja kwa wageni hao kutaongeza mapato yatokanayo na utalii na kukuza uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

Mratibu wa Majiji hayo kwa upande wa Humburg, Jinken Bruns, alisema ushirikiano wao na Dar es Salaam ni muhimu na wamekuja nchini kuongeza ushirikiano katika sekta hizo.

Alisema wamekuwa wakifanya kazi pamoja katika sekta mbalimbali katika kuongeza umoja na ushirikiano wa majiji hayo ili kuhakikisha yanapiga hatua kubwa kiuchumi.

"Nimefurahi sana kuwa Dar es Salaam, katika ushirikiano wetu, huu ni mji mzuri wenye vivutio vya kutosha, ninaamini tutajifunza mambo mengi mazuri," alisema.

Mwenyekiti wa Wadau wa Jiji la Dar es Salaam, Michael Onesmo, alimpongeza Meya Kumbilamoto kwa ushirikiano na jiji hilo.

Alisema lengo ni kuangalia sekta zote za kiuchumi na uhusiano wao unavyoweza kuongeza mapato na uchumi wa majiji hayo.

Alisema kukutana na watu wa majiji hayo ni fursa ya kuona namna yanaweza kuchangia uchumi wa mataifa hayo.

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Tukarabati viwanja hivi lakini tufikirie



**Na Joseph Kulangwa**

MIAKA ya 70 nikiwa sekondari Mwanza, tulitakiwa kwenda pale Kirumba, kwamba siku hiyo, Waziri Mkuu, Edward Sokoine, alikuwa anakwenda kuweka jiwe la msingi la uwanja wa michezo.

Huo ni uwanja ambao leo unajulikana kama CCM Kirumba. Siku hiyo asubuhi tulitakiwa tufike mapema na mgeni rasmi akifika atukute eneo la tukio.

Na kweli siku ilipofika tukawahi pale na alipokuja mgeni akazungumza na wananchi tukiwamo sisi wanafunzi wa shule za Mwanza na kisha akaweka jiwe la msingi nasi tukashiriki kupanga matofali, akaondoka.

Ujenzi wa uwanja huo ukaenda kasi na ukakamilika baada ya miaka kadhaa hivi. Ukawa mmoja wa viwanja vikubwa vya michezo nchini na kusaidiana na Uwanja wa Taifa enzi hizo ambao ni wa Uhuru leo mkoani Dar es Salaam.

Uliitwa uwanja wa CCM Kirumba hata mfumo wa vyama vingi vya siasa uliporejea nchini mwaka 1992 bado ukaendelea kuwa uwanja wa CCM licha ya kujengwa na wananchi wasio na walio wa CCM.

Kumbe CCM iliamua kuchukua viwanja vyote vya michezo vilivyojengwa na wananchi na kuvifanya miradi yake, huku vyama vipya vya upinzani vikibaki havina kitu licha ya baadhi ya wanachama wao kushiriki ujenzi wa viwanja hivyo.

Nimeikumbuka hii, baada ya hivi karibuni kusikia bungeni kuwa zitatengwa Sh. bilioni 10 kwa ajili ya ukarabati wa baadhi ya viwanja vya michezo nchini, ili kukaa sawa kwa maandalizi ya Tanzania siku moja kuwa mwenyeji wa michuano ya soka ya Afrika, AFCON.

Tamko hilo lilizua gumzo kubwa nchini huku watu wakihoji, nikiwamo mimi, kwamba viwanja hivyo vingi ni mali ya CCM ambacho ni chama kama vilivyo vingine vya CUF, ACT-Wazalendo, NCCR-Mageuzi, Chadema na vingine.

Inafikirisha sana, kuona ni kwa nini itumike kodi ya wananchi kukarabati viwanja vya chama kimoja cha siasa, hata kama ni tawala, kwa sababu mapato yapatikanayo kwenye mechi hayaendi kwenye vyama vyote.

Hivi ikitokea mathalan Chadema ikaiomba serikali itenge fedha kwa ajili ya kupaka rangi kwenye jengo la makao makuu yake pale Kinondoni, kweli hata bungeni hoja hiyo itafika? Sidhani! Au CUF ikafanye mkutano wake CCM Mkwakwani bila kulipa!

Ninakumbuka enzi za Dk. John Magufuli akifanya kampeni, alipata kusema eneo likimchagua mpinzani halitapelekewa maendeleo. Nikajiuliza hivi wapinzani kumbe si Watanzania na wala hawana muunganiko na yao?

Nikasema hapana, halikuwa jambo jema kutoa kauli kama hii tena kwa kiongozi mkubwa kwani ni kama kutotendana haki fulani hivi, na ni uporaji haki ya mpinzani katika nchi yake, kwamba akichaguliwa mathalan ubunge basi hilo jimbo lisahau maendeleo.

Ni kweli kuna maeneo ambako wananchi waliona ni kweli CCM inaongoza vizuri lakini diwani, lazima atoke upinzani kutokana na uwezo wake binafsi. Na kweli walipofanya hivyo, kwa kuchagua diwani mpinzani, jimbo likatelekezwa.

Mbaya zaidi hata mbunge aliyechaguliwa na wananchi hao hao, waliochagua diwani mpinzani, naye akawapa kisogo, akaacha kabisa kuzungumzia maendeleo katika jimbo husika. Nilishangaa sana.

Hii ndiyo sababu kuibuka hoja ya kwa nini serikali ipeleke fedha za walipakodi kwenye viwanja vya CCM kana kwamba fedha zipatikanazo katika viwanja hivyo, zinakwenda kwenye ruzuku ya vyama hivyo vya upinzani.

Si siri kuwa CCM ilipata fursa ya kumiliki viwanja hivyo na miradi mingine kutokana na kuwa mikononi mwa TANU awali, kabla na hata baada ya muungano wa TANU na ASP mwaka 1977.

Busara ingetumika kwamba zilizokuwa mali za chama wakati huo, zingerejeshwa kwenye halmashauri za miji au majiji husika na hivyo kuwa mikononi mwa wananchi, badala ya chama, bila shaka malalamiko haya ya kwa nini viwanja vya CCM, yangetoweka.

Hebu fikiria tuliojenga uwanja wa Kirumba enzi hizo na leo baadhi yetu wako upinzani wanajisikiaje kunyang'anywa jasho lao walilotoa enzi hizo? Busara itumike tu, miradi hii irejeshwe mikononi mwa wananchi na si mwa chama. **Alamsiki!**

# ATHARI HASI ZA WANANDOA KUISHI MBALI NA FAMILIA



NDOA ni taasisi ya kijamii ambayo ni kitovu cha familia na malezi. Mungu alikuwa na kusudi kamili la kuanzisha ndoa. Mungu alianzisha taasisi ya ndoa ili wanandoa waishi pamoja kwa umoja, kuendeleza uumbaji wake, kusaidiana, kushirikiana, kutawala na kumiliki. Ni mpango wa Mungu toka mwanzo kuwa mwanamume na mwanamke waishi pamoja katika ndoa ili kukua pamoja na kufurahishana.

Mwanadamu anaweza kuwa na mtu wa karibu wa kushirikiana naye katika mambo mengi lakini kuna mambo mengine ambayo hawezi kushirikiana naye.

Mungu aliona mwanamume anahitaji msaidizi atakayemfanya kuwa na ushirika mkamilifu. Msaidizi katika utoaji wa ushirika huo ni mwanamke kupitia ndoa. Ushirika huu una kibali cha Mungu na umezingatia agizo la Mungu linalowataka wanandoa kuishi pamoja kwa umoja ili waondokane na upweke na ubinafsi.

Ni mpango kamili wa Mungu kwamba wanandoa waishi pamoja kwa umoja katika maisha yao.

Kuishi kwa umoja huwaondoa wanandoa katika dhambi ya ubinafsi miongoni mwao na kushirikiana vyema katika majaliwa yao na kuwa kitu kimoja katika hali zote.

Umoja huu unapaswa kuonekana katika maneno na matendo ya wanandoa.

Kwa mantiki hii, ni muhimu kufahamu kuwa kitendo cha wanandoa kuishi mbali na familia zao ni kinyume cha kusudi la Mungu. Wanandoa wanapoishi mbalimbali huleta majaribu yanayozaa uasi, usaliti na kubomoa ustawi wa familia.

**KAZI NA FAMILIA**

Upo uhusiano wa karibu kati ya familia na kazi zetu. Kazi zinahitaji familia na familia zinahitaji kazi. Mafaniko katika kazi yanategemea furaha na usalama wa familia.

Kwa mantiki hii, ni muhimu upangaji wa vituo vya kazi na hamisho za watumishi mahali pa kazi uzingatie ustawi wa familia.

Waajiri wasiojali ustawi wa familia kwa sehemu kubwa huchangia uwapo wa migogoro ya ndoa na kuondosha furaha ya mtumishi mahali pa kazi.

Watu wengi kazi zimewatenga na familia zao. Ninapozungumzia familia katika makala hii nina maana ya baba, mama na watoto.

Tunashuhudia leo baadhi ya watumishi wanandoa wanaoishi mbali na familia zao.

Kwa mfano; unakuta kituo cha kazi cha mume kipo mkoani Pwani huku kituo cha kazi cha mke kipo mkoani Kigoma au Mume anaishi Njombe na mke anaishi Arusha, na wengine mke anaishi Mbeya na mume anaishi Dodoma; mwingine anaishi Mafia, mwingine yuko Dar es Salaam au nje ya nchi. Kwa namna yoyote ile umbali wa jinsi hii hauwezi kuiacha familia salama sana.

**ATHARI HASI KUISHI MBALI NA FAMILIA**

Kitendo cha mume au mke kuishi mbali na mwenzi wake ni kikwazo kikubwa na mtihani mzito. Mara nyingi hali hii imeleta vishawishi na kuathiri uhusiano wa wanandoa wengi kwa sababu ya matatizo yanayozalishwa na umbali.

Umbali na hali ya upweke vimechochea baadhi ya wanandoa kuanzisha uhusiano mpya nje ya ndoa ikiwa ni sehemu ya kufidia pengo la umbali. Waathirika wakubwa katika hali hii huwa ni wanawake na watoto.

Uhusiano huu ukiishakolea na kuota mizizi, husababisha mwanandoa kupoteza mvuto na thamani ya mwenzi wake. Hali hii hutengeneza mazingira ya migogoro isiyo ya lazima katika ndoa.

Baadhi ya ndoa zimebaki kuwa za heshima tu na kupoteza uhalisia wake. Athari zake ni kubwa kwa wanandoa wenyewe na watoto waliozaliwa katika ndoa hizo.

Wako wanandoa ambao wamevurugwa, wamejeruhiwa nafsi na ndoa kuvunjika kwa sababu ya kuishi mbali na wenzi wao.

Wanandoa wanapoishi huyu huku na huyu kule huongeza gharama za maisha, hali ambayo huathiri tabia na mienendo yao. Umbali husababisha msongo wa mawazo ambao huathiri afya ya akili na mwili; hupunguza kiwango cha mshikamano wa wanandoa, mvuto, upendo na joto la ndoa.

Mume na mke wanapoishi mbalimbali, huathiri watoto kisaikolojia na kimakuzi kwa sababu ya kukosa malezi ya wazazi wote wawili.

Thamani na umuhimu wa mzazi kwa watoto wake unategemea matunzo wanayopata na ukaribu alionao kwao.

Mara nyingi watoto huonyesha upendo na kumthamini mzazi mwenye muda nao. Wako watoto ambao wamewachukia wazazi wao na kupoteza mvuto na baba au mama au wote kwa pamoja kwa sababu ya kuhisi kutokupendwa, kupuuzwa na kutelekezwa

Malezi mabaya ya watoto ni chanzo cha mmomonyoko wa maadili na uzao wa watu katili katika jamii.

Ninatambua kuwa utumishi ni popote, na kwamba mazingira ya kikazi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za kazi huweza kulazimu mume au mke kuishi mbali na familia yake.

Hata hivyo, upo umuhimu mkubwa kutafakari kwa makini na kulipa uzito unaostahili suala hili kwa kuzingatia kuwa wako watumishi wanandoa waliopangwa vituo vya kazi lakini hawana furaha ya kazi zao na maisha yao.

Ufanisi wa utendaji wao wa kazi umeshuka na kuleta athari mahali pa kazi.

Hali hii hujitokeza kwa kuwa mtumishi anatumia muda wake mwingi zaidi kufikiri kuhusu familia na matatizo ya nyumbani kwake kuliko kazi.

Kwa kuzingatia mazingira halisi wanayokutana nayo baadhi ya watumishi wanandoa wanaoishi mbali na familia zao, ninatoa ushauri kwa waajiri wote nchini kuchukua hatua za makusudi ili kurekebisha hali iliyopo sasa.

Ni muhimu zitungwe sheria na kanuni zenye lengo la kuweka utaratibu mzuri zaidi utakaolinda ndoa na ustawi familia kwa madhumuni ya kuongeza tija na utendaji wenye ufanisi mahali pa kazi. Mwanandoa anayetamani kuishi mbali na mwenzi wake atakuwa anatafuta matakwa yake. Halikadhalika, ukiona baba au mama umepoteza mvuto na umuhimu kwa familia yako kiasi cha familia kutokutamani uwapo wako, ujue una matatizo yanayohitaji kufanyiwa kazi.

**NDOA NI MSINGI WA FAMILIA, JAMII NA TAIFA**

Ndoa ni kitovu na msingi wa familia, jamii, Taifa na maendeleo yake. Msingi wa ndoa ukiyumba, kila kitu kitayumba. Kazi zitayumba, ustawi wa familia utayumba, jamii itayumba, Taifa litayumba na maendeleo yatayumba kwa sababu ya kukosekana kwa nguvu kazi yenye utulivu na amani. Furaha na amani ya mtumishi ni chachu ya mafanikio mahali pa kazi na maendeleo.

Ndoto na matumaini ya kila mmoja wetu wakati anapofunga ndoa, huwa ni kufanikiwa na kuishi maisha yaliyojaa upendo, furaha na amani.

Amani katika ndoa hujengwa, upendo na furaha hutengenezwa kwa kauli na matendo mema ya mume na mke.

Mungu alianzisha taasisi ya ndoa ili mume na mke waishi pamoja kwa furaha.Mafanikio na baraka katika kazi zetu huanzia nyumbani. Mafanikio na baraka hizi hudhihirika pale panapokuwapo furaha, utulivu na amani nyumbani.

Nyumbani kukiwa vizuri,upo uwezekano mkubwa kazini kukawa vizuri pia.

Kazi zipo ili kuleta furaha na sio kuleta upweke na maumivu. Kwa hiyo, ni muhimu kufanya kazi kwa bidii ili kupata fedha, lakini kazi isiwe sababu ya kudumu ya kuondoa utu na thamani yako kwa familia. Mungu akubariki!

**■Dk. Enock Emmanuel Mlyuka ni Mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online.**

**Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066].**


# MAISHA

JULAI 3, 2022
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili



Ukurasa 13

**Kuwa mjanja pensi zinavyofurahisha**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**

Mambo ya msingi kuzingatiwa unaposafisha choo cha nyumba



Ukurasa 12

**HARUSI**



**KUTOBOA SIKIO**


# Urembo wa kale unaopendwa

Ukurasa 14

## WATOTO


### MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | P | W | A | N | I |
| ■ | O | ■ | ■ | Y | ■ |
| A | L | A | ■ | U | ■ |
| ■ | I | ■ | I | M | O |
| ■ | S | ■ | ■ | B | ■ |
| K | I | N | D | A | ■ |


## AMSHA AKILI





## TOA TOFAUTI 5




## PAKA RANGI




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
UGA, UDA, PENDO, SANDA, PAGAWA, DANDIA




Alichokifanya daktari

MTOTO Karim alirudi mapema nyumbani baada ya mwalimu kuwaruhusu kwa ajili ya kujiandaa na mitihani yao ya wiki.

Aliporudi nyumbani alimkuta mama yake akipika chakula cha jioni katika jiko la mkaa. Alimwendea mama yake jikoni na kuanza kumuuliza maswali.

**Karim:** Mama leo mwalimu katufananisha na huu moto sijui kwa nini?

**Mama:** Mimi sijui unachomaanisha, niambie basi

**Karim:** Katuambia eti akilizetu zipo kama chuma, tukitaka kutengeneza jembe au panga lazima kipite kwenye tanuri la moto.

**Mama:** Mwalimu yupo sawa kabisa, hapo anamaanisha kwamba ukitaka kufanikiwa lazima utumie nguvu ya kiakili kutafuta mbinu za kupata kile unachohitaji.

**Karim:** Kumbe mama ni hivyo, basi mimi nitatumia nguvu katika masomo yangu.

**SWALI**

Matunda ya parachichi yanalimwa katika maeneo yenye hali gani ya hewa?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Simulizi Pazi alivyoserebuka kimaisha

***KARIBU tena msomaji wangu katika safu yetu hii ya Maisha Ndivyo Yalivyo. Leo nikuletee simulizi nzuri ya kimaisha iliyotokea mwaka 1974 lakini ina fundisho kubwa sana kwa vijana wa kizazi cha sasa.***

Simulizi hii alinisimulia hivi karibuni msomaji mahiri wa Nipashe, mzee Hadilonga Ding'alonga Dina Mbuli wa Buguruni Makukula jijini Dar es Salaam. Msikie Pazi ndoa ilivyomtoa kijasho chembamba!

Pazi anasema: Mwaka 1974 niliajiriwa kiwanda cha Blanketi, barabara ya Migeyo jijini Dar es Salaam. Baada ya mwaka mmoja nikapewa likizo, nikarudi kijijini kwetu Mwanarumango Boga.

Nilipokewa na ndugu zangu kwa furaha kubwa, nilibeba zawadi nyingi, mojawapo ilikuwa mikate ya Siha. Ilikuwa inatengenezwa Buguruni kwa Kimbengele, kuvuka njia ya treni.

Nilipofika nyumbani wazazi walinikaribisha kwa lugha ya nyumbani kwetu, 'mwenetu kubwela'. Niliketi kwenye kiti cha malimba, bibi na babu walikuwapo. Na kabla ya kuja nyumbani wakati nikiwa kazini, wazazi walishanitafutia mchumba.

Hivyo, nilipopewa likizo tu, sikufanya ajizi. Asubuhi babu na baba mdogo na kaka wakaenda kwa wazazi wa mchumba, alikuwa ni mwali ndani yaani kaalikwa na hiyo ni mila za watu wa Pwani ambao ni Wazaramo, Waluguru, Wakware, Wazigua.

Wazee wakapokewa wakawekewa jamvi, mjadala ukaanza. Wakati wote huo, kaka wa yule dada yupo pembeni kashika debe na kama kifimbo hivi. Wale wazee walipoanza kujadili posa ya binti yao, kaka akaanza kupiga lile debe na sauti ya lile debe likawa linapoteza mawasiliano.

Wakinyamaza naye ananyamaza. Wakianza kujadili tu naye anapiga debe lake na wazee wakakumbuka kuna pesa ya kaka Gumba la Mlam. Akapewa alivyopewa ndipo akaondoka huku wakitoa posa! Wakaagana. Posa wakati ule ilikuwa Sh. 300 tu.

Baada ya yote hayo kukamilika, sasa ni maandalizi ya kumtoa mwali. Mimi likizo imeisha nikarudi mjini kuanza kazi. Nikawaachia hekaheka kutafuta ngoma vikundi kama vitatu; mdundiko wa Buguruni kwa Mnyamani, Wa Mzee Kifimbo. Mkwajungoma wa Njenje, Tokomile la Mzee Kambangwa. Mzee Kindemile, Mzee Minziha wa Tabata Segerea.

Muda wa kumtoa mwali ukafika sherehe ilikuwa kubwa wakati ule ujishike ni gharama sana! Shughuli ikaisha nikasubiri tu mimi nikaoe. Pale kazini nikaomba likizo fupi maana mjomba wa mwali alishaanza kulalamika kwamba mwali kachezwa muda mrefu yuko gizani.

Mimi nikapanda basi kwenda Mwanalumango kwa Boga. Nikafika nyumbani na kesho yake asubuhi ikaandaliwa harusi kama ilivyo ada. Kukutana na binti ikatokea sintofahamu. Kila nikimuuliza swali hakubali. Ndipo bibi akaniomba mke wangu amsindikize Buguruni kwa Mnyamani.

Mimi nikamruhusu kumbe walikwenda kwa mtaalamu kutizamia kwa nini binti miezi sita hashiki ujauzito? Kufika kule bibi akamweleza binti wanakokwenda ni kwa mtaalamu kuangalia tatizo lipo wapi.

Binti akasema ni sawa, wakaingia ndani wakakaribishwa. Mtaalamu akaanza vijimambo vyake! Akaanza kuelezea safari yao ilivyo. Akawaambia mko wawili lakini wewe binti una matatizo yako.

Siku iliyofuata nikarudi mjini, bibie akabaki kumalizia darasa la saba. Siku ya nane kaka akaenda Posta kunipigia simu niwasubiri stendi ya mabasi Buguruni kwa Mnyamani. Ilikuwa siku ya Jumamosi. Nikawapokea amesindikizwa na dada yangu mdogo wakati huo nilipanga Ilala Mtaa wa Sharifu Shamba.

Maisha tuliyaanza kwa mbwembwe. Bibi mwenye nyumba alikuwa Mpogoro. Akanishauri anikatie kijishamba kule Spengo ili baadhi ya mahitaji tusinunue. Miezi sita imeisha bibie hata dalili za ujauzito hamna! Mh! Hii sasa balaa.

Bibi mwenye nyumba naye akapata mshtuko kulikoni? Bibi mwenye nyumba alitokea kumpenda sana ila sasa akaanza kumbana, tatizo hushiki ujauzito. Na aliyefanya hivi ni kijana wa kijijini kwenu aliyetaka kukuoa wewe ukamkataa. Na sasa anakutafuta ajue unakaa wapi. Bibi akamuuliza, ni kweli anavyosema?

Wakarudi lakini binti hakuwa na amani ikabidi amuulize; kwani mlienda wapi na bibi? Binti akaanza kulia. Kwa nini husemi? Kama husemi kesho jiandae twende nyumbani. Bibi kusikia akaja na kueleza hali halisi.

***Mpenzi msomaji, bila shaka umeanza kupata picha kuhusu mtiririko wa kisa hiki cha kweli. Ni simulizi nzuri inayoelezea mitihani kabla ya ndoa, baada ya ndoa na mwisho mbaya wa ndoa. Itaendelea wiki ijayo. Una maoni? Ujumbe 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Manispaa, TRA wachukue hatua kudhibiti hoteli hizi

UNAPOSAFIRI kwa basi kwenda mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Kati na Kanda ya Ziwa, lazima utapita mkoani Morogoro na kwa wanaotumia magari ya alfajiri kwenda Songea, Njombe, Mbeya na Ruvuma lazima wanasimama kupata kifungua kinywa kwenye 'Mji Kasoro Bahari'.

Kwa wanaokwenda Mwanza, Musoma, Shinyanga, Bukoba, Kahama na kwingine kwa mwelekeo huo wanapotoka Dar es Salaam, kituo cha kwanza kwa ajili ya huduma za kijamii ni mjini Morogoro.

Kama hilo haitoshi, wanaokwenda mikoa ya jirani kama Dodoma hasa kwa magari yasiyo ya alfajiri, wanasimama kupata chakula cha mchana au cha jioni kwenye moja ya hoteli za mkoa huo kutegemeana na makubaliano baina ya dereva na wamiliki wa hoteli.

Kwa ujumla, unaposafiri kwenda mikoa mingine hususan ya Kanda ya Kaskazini na Kusini huduma za vyakula ni za kuridhisha sana kuanzia usafi wa eneo husika na vyakula, lakini siyo kwa njia ya Morogoro.

Hoteli zote ambazo mabasi yanasimama ili abiria 'wachimbe dawa', wapate huduma ya chakula na mapumziko kwa ujumla siyo za kuridhisha kabisa, hali inayozua maswali mengi kwa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kwamba huwa haioni hayo yote?

Kuanzia huduma ya vyoo ni kuchafu na vibovu kiasi cha kuziweka hatarini afya za wasafiri kwa kuwa hakuna anayefuatilia, mwenye biashara huamua anavyotaka kwa kuwa hakuna ukaguzi.

Vyakula vinauzwa bei ya juu, vinywaji vinauzwa mara mbili hadi tatu ya bei na wakati mwingine abiria ananunua kwa kuwa anahitaji na ndilo eneo pekee alilofikishwa na dereva wa basi husika.

Ninatambua kwenye kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuna Ofisa Afya ambaye moja ya majukumu yake ni kufuatilia usafi wa maeneo yote ya biashara, hasa hoteli na migahawa inayotumiwa na watu wengi, kisha kuchukua hatua, ikiwamo kufunga biashara husika kwa anayebainika kutokidhi vigezo.

Migahawa na hoteli ninayoizungumzia mjini Morogoro iko kilomita chache kutoka iliko Manispaa ya Morogoro. Swali ninalojiuliza wanafanya ukaguzi hadi kwenye vyoo, wanaona vingine havina milango na ni chakavu kupita kiasi au wanaacha bora liende na kukusanya kodi pekee?

Ni muhimu sana Manispaa ya Morogoro ikajali afya za wananchi, kama ambavyo maeneo hayo yanawaingizia fedha kama chanzo cha mapato, wanao wajibu wa msingi kufuatilia huduma zinazotolewa humo kama zinaridhisha.

Ni lazima hatua zichukuliwe ili mazingira ya hoteli na migahawa iboreshwe au kujengwa upya. Kama mtu anataka kuwekeza kwenye huduma hizo, afanye uwekezaji wa kuridhisha na kukidhi vigezo vyote vya afya kuliko wananchi kuingizwa kwenye matatizo.

Kama maeneo haya wanatoza fedha zaidi ya bei halisi ya bidhaa husika, kwanini wanashindwa kuboresha maeneo yakawa mazuri na ya kuridhisha kuanzia huduma za vyoo, chakula na vinywaji?

Maana yake ni kwamba hakuna ufuatiliaji wa serikali, ndiyo maana kimebaki kuwa chanzo cha mapato pekee pasi na ufuatiliaji wa kama huduma zinazotolewa zinakidhi matakwa ya kiafya kwa mujibu wa sheria.

> **“Kama maeneo haya wanatoza fedha zaidi ya bei halisi ya bidhaa husika, kwanini wanashindwa kuboresha maeneo yakawa mazuri na ya kuridhisha kuanzia huduma za vyoo, chakula na vinywaji?**

Wasafiri ni watoto, vijana, umri wa kati na wazee ambao ni mchanganyiko wa wanaume na wanawake, wote wanatumia vyoo visivyoridhisha na ambao wako hatarini kupata maradhi ya njia ya haja ndogo ni wanawake na watoto.

Lazima hatua zichukuliwe tuone mabadiliko kuliko kuachwa ilivyo, serikali isiishie kukusanya mapato pekee, bali kujiridhisha na kusimamia usafi wa maeneo husika. Kama inashindikana wachukue hatua kwa mujibu wa sheria.


Hoteli nyingi za Kanda ya Kaskazini mteja anaponunua chochote anapewa stakabadhi ya EFD, lakini kwa hizi za Manispaa ya Morogoro, kwa uzoefu wangu wa kusafiri njia hiyo sijawahi kupewa stakabidhi, maana yake hata Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapoteza mamilioni ya shilingi ambayo yangeingia kwenye kapu la Taifa na kutekeleza miradi ya maendeleo.

Kama hoteli za Kamda ya Kaskazini imewezekana kuweka mashine za EFD, basi hata Morogoro na mikoa mingine ambayo mamia ya wasafiri hutumia huduma, kuwe stakabadhi hizo muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

***Mungu ibariki Tanzania***

# HARUSI







Juni 25, ilikuwa siku ya kukumbukwa na yenye furaha kwa Jackson Noel na Rosada Thomas, baada ya kufunga ndoa katikakanisa la Tabata Msimbazi na kufatiwa na tafrija yakuwapongeza maharusi iliyofanyika ukumbi wa BarakudaTabata jijini Dar es Salaam.





# MITINDO











KUWA MJANJA

## Pensi zinavyofurahisha

JE unataka kuwa mjanja kwa kuvaa nguo inayokupa furaha wakati wa likizo au mapumziko?

Basi usipate tabu kufikiria, kwani kaptula au pensi ni vazi zuri kulitumia wakati ukiwa umepumzika baada ya juma zima la kuwajibika.

Hata hivyo, ili uwe na mwonekano wa kipekee ni lazima kujua mwongozo wa jinsi ya kuvaa vazi hilo fupi.

Ni muhimu kufahamu urefu gani sahihi kwako, jinsi ya kuzichanganya na rangi na viatu gani vinafaa kuvaliwa.

Vazi la kaptula ni maalum kwa ajili ya kipindi cha joto, kwani linaacha sehemu kubwa ya mwili kuwa wazi.

Kwa wanaume inapendeza kuvaa kaptula zenye urefu wa wastani ambao haupiti chini ya magoti. Hii inampa mtu uhuru wa kutembea bila hofu sehemu tofauti ambazo kimsingi vazi hilo linaruhusiwa.

Ni muhimu kuwa na mtindo wa kisasa kwa sababu dunia ya mitindo inakwenda kwa kasi, kila siku inabuniwa aina mpya na hivyo unatakiwa kuwa makini kila wakati.

Inapendeza zaidi kuchagua viatu sahihi vinavyoendana na vazi lako, Hapa unatakiwa kuvaa viatu vya wazi, raba au viatu aina ya buti zenye shingo fupi.



UREMBO

KUTOBOA SIKIO

# Urembo wa kale unaopendwa

UREMBO ni asili ya wanawake, idadi kubwa wanapenda kujiremba kwa kutoboa masikio kwa ajili ya kuvaa hereni.

Hata hivyo urembo wa kutoboa sikio unaweza kupata matatizo ya kuvimbia na kusababisha madhara. Leo tuangalie ni njia zipi unapaswa kuzifuata ili usipate madhara unapotoboa sikio.

**Mambo ya kuzingatia**

Mosi usiguse sikio kwa maji angalau siku saba baada ya kutoboa, liguse kwa kutumia mafuta ya mgando mara kwa mara.

Hakikisha unazungusha kama ni uzi au hereni uliyotobolea sikio kila siku ili nyama ya sikio isikandamizane na kusababisha madhara.

Epuka kuvaa hereni ambazo si salama kama zenye kutu, zilizokaa muda mrefu na za plastiki muda mfupi baada ya kutoboa.

Hakikisha masikio yako yamekauka ndipo uvae hereni halisi ambazo hazitakuletea madhara.

Ukiona una dalili ya kupata usaha au masikio kuanza kuuma, osha na maji safi ya uvuguvugu uyaweke chumvi kidogo na kisha ukaushe kwa kitambaa laini kikavu na upake mafuta ya nazi.

Unaweza kumuona daktari kama tatizo litaendelea kuwa kubwa.



MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Biringanya ya nazi

UNAWEZA kuona mboga hii ni ya kawaida na umezoea kula nyumbani kila siku kutokana na kutokuwa na gharama kubwa.

Hata hivyo, chakula hiki ni salama kwa afya yako kutokana na kuwa na faida lukuki zinazopatikana.

**Mahitaji**

Nyanya chungu fungu kubwa moja, bamia fungu moja, biringanya kubwa tatu, pilipili hoho nusu, kitunguu kikubwa kimoja, karoti nusu, nazi mbili, nyanya nne na mafuta kidogo.

Mahitaji mengine ni binzari kiasi kama ukipenda, chumvi kiasi na pilipili mbuzi moja kama wewe ni mtumiaji.

**Jinsi ya kuandaa hatua kwa hatua**

Andaa nyanya, nyanyachungu, bamia na biringanya zako, kwa kuziosha vizuri kwa maji safi. Kisha zimenye na kuzikata biringanya, bamia, nyanyachungu na kuziweka kwenye sahani tayari kwa mapishi.

Andaa hoho, karoti, vitunguu na nazi ikune kabisa, uchuje tui zito.

Bandika sufuria jikoni weka mafuta, yakipata moto tia vitunguu ukaange, vikibadilika rangi tia hoho endelea kukaanga kidogo kisha tia nyanya ukaange.



Mimina nyanyachungu na biringanya na bamia zako na umimine tui la nazi.

Tia karoti, chumvi, binzari na usisahau kutupia kapilipili mbuzi ukipenda, koroga uache mchuzi uchemke na nyanyachungu na biringanya zetu ziive. Zikishaiva mboga yetu itakuwa tayari.

Mboga hii unaweza kula kwa ugali, wali au chakula kingine unachopendelea.

**Faida za biringanya**

Hutumika kutibu vidonda vya tumbo, kwa wale ambao wanasumbuliwa na tatizo hili, husaidia kupata usingizi mzuri kwa wale ambao wana tatizo la kukosa usingizi.

Kadhalika husaidia kwa kiwango kikubwa kuondoa sumu zilizomo katika mwili wa mwanadamu.

MAISHA NI NYUMBA
Na Elizabeth Zaya



# Mambo ya msingi kuzingatiwa unaposafisha choo cha nyumba

USAFI wa nyumba wa mara kwa mara ni nguzo kubwa ya kuistawisha na kuipendezesha, na isipofanyiwa usafi wa uhakika, huchakaa mapema na hata kuharibika kabisa.

Leo ninapenda kuzungumza baadhi ya dondoo za namna ya kusafisha bafu na choo.

Kabla ya kuanza kusafisha bafuni, kwanza ondoa vitu vyote vya kuhamishika, wakati huo ukihakikisha dirisha liko wazi ili hewa ipite kuondoa hewa nzito.

Baada ya hapo, ondoa buibui kwenye kona zote za dari ikifuatiwa na kufuta vumbi mlango, sehemu za ndani na nje.

Wakati wa kusafisha ni vyema kuanzia juu kushuka chini ili kuruhusu taka za vumbi na buibui zimwagike sakafuni kwa ajili ya kisafisha mwishoni.

Weka dawa ya kusafishia katika sehemu zenye uchafu ili iwe rahisi wakati unasugua.

Ni vyema ukazingatia maelezo ya dawa ya kusafishia ili kuwa na uhakika unatumia kiasi sahihi ambacho hakiwezi kuharibu.

Katika kuta za bafu pia unapaswa kupaka sabuni au dawa nyingine za kusafishia endapo zitakuwa ni za marumaru, na kwa kutumia sponji ama brashi unaweza sugua sehemu uliyoweka sabuni hiyo huku ukihakikisha unaiisuuza kuondoa michirizi yote michafu, na kama ukuta ni wa karibia na sinki ama bakuli la choo, ukaushe kwa taulo.

Ni muhimu kukumbuka kuvaa glovu wakati wa kusugua kwani baadhi ya dawa na sabuni zinaweza kuchubua ngozi.

Safisha kioo kwa kutumia maji na taulo au dawa ya kusafishia vioo na taulo.

Safisha nje ya choo ukianza na ile sehemu ya juu ya kuvuta maji, kwa taratibu unaweza kuendelea kusafisha eneo lote la nje ya choo ambalo ni pamoja na mfuniko na eneo la chini ya sehemu ya kukalia na kupafuta kwa taulo.

Kwa upande wa sakafu, hakikisha usafi wako unaanzia sehemu zilizojificha hadi zile za wazi na ni vyema kusafisha vumbi na uchafu wote ulio chini eneo la choo lilipoungania na sakafu.





## Namna ya kutunza jokofu nyumbani



MATUMIZI ya jokofu ndani ya nyumba ni jambo muhimu kutokana na kuhifadhi vyakula na matunda yasiharibike. Pia chombo hiki kina kazi ya kupoza maji na vinywaji mbalimbali kwa lengo la kukupa furaha.

Hata hivyo, wengi hawafahamu namna ya utunzaji wake ili jokofu lidumu kwa muda mrefu. Hizi ni baadhi ya dondoo ambazo zinaweza kukusaidia katika utunzaji.


**1.** Usafi wa koili husaidia kuhakikisha kifaa kinafanya kazi kwa ufanisi. Unaweza kusafisha angalau mara mbili kwa mwaka koili zile zinazokuwa nyuma kwa kutumia brashi laini.

**2.** Umbali kutoka ukutani unaweza kuwa ni chanzo cha kukosekana hewa ya kusaidia upoozaji.Nyakati zote hakikisha jokofu lako lipo umbali wa kutosha kutoka kitu chochote ambacho kitazuia kwa namna yeyote ile mzunguko wa hewa wa kutosha.

**3.** Mipira ya milango unaposafisha Jokofu lako hakikisha milango na mipira ya kwenye mlango wa kifaa hiki inakuwa safi kwa kuzuia jokofu kushindwa kutunza ubaridi.

**4.** Kuyeyusha kila kitu angalau mara mbili kwa mwaka kutasaidia kuongeza ufanisi wa jokofu.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
PATO
'PAMBA' NAULI, UMEME, KODI, ULINZI, TAKA, MAJI, KARO YA SHULE DHARURA BAR, MSOSI 'SMOLU HAUSI' VOCHA
TUONGEE UKWELI, HIVI LILE NI KOMBE AU BLENDA YA KUSAGIA JUISI?
HA HA HAAAA HA HA HA HAAA JAMANIEEE LITAKUFA JITU MWAKA HUU KWA KIWEWE HA HAAA
SASA MBONA ILE DAWA NIMEKUNYWA LAKINI NILIPOTAKA KUIBA MCHANA WAMENIONA?
UNGEENDELEA UONE MWISHO WAKE
KONDA KATA MBILI, NA HUYU DADA MWENYE KIJORA KILICHO BANA NA KOPE NDEFU
KAKA JIHESHIMI!
KWAN NAN?
WEWE MTU AMEKULIPIA NAULI SEMA ASANTE...
JAMANI WENGINE WAKE ZETU HUMU
ULITUMWA UKAE NAE MBALI?
GUD!
ANAWATEGA WATU ILI APIGANE
KWA HII HATUFIKI MBALI NITAPIGA MTU
JIKOKOTE UKAANGUKIE KWINGINE VIJANA WA MTAA HUU SIO WATU
UNADHANI WATANIFANYIA KAMA JANA? WAJE TENA LEO WAONE!
ABIRIA MIMI NI MUME WA MTU USINIKUMBATIE MKE WANGU HATONIELEWA TUTAPATA AJALI MBAYA
BABUWEEEE SEMA MOJA, AJALI AU MKEO? MBONA MBABAIFU?
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...KAMA UMEMUACHA, KAOLEWA UNAMNUNIA NANI?

HABARI KIMATAIFA

## Watu 26 wafariki kutokana na maporomoko ya ardhi nchini India

Vikosi vya uokoaji vimefanikiwa kupata miili ya watu 26 waliofariki kutokana na maporomoko ya udongo yaliyoharibu kabisa kituo cha ujenzi wa reli kaskazini mashariki mwa India.

Kazi ya uokoaji inatarajiwa kuendelea kwa siku kadhaa, lakini kuna matumaini hafifu ya kupatikana kwa manusura kati ya watu 37 ambao hawajulikani walipo tangu siku ya Jumatano.

Ofisa wa uokoaji, Pankaj Kavidayal, alisema watu 21 kati ya 26, waliothibitishwa kufariki walikuwa wanajeshi waliopelekwa eneo hilo kutoa ulinzi kwa maofisa wa reli kutokana na miongo kadhaa ya uasi wa makundi ya kikabila yanayotaka kujitenga katika eneo hilo.

Tangu Mei 17 mwaka huu, takriban watu 200 wamepoteza maisha kutokana na mafuriko katika majimbo ya Assam, Manipur, Tripura na Sikkim nchini India, huku wengine 42 wakifariki nchini Bangladesh.

Wanasayansi wanasema mabadiliko ya hali ya hewa ndio chanzo cha hali hiyo isiyokuwa ya kawaida.

**DW**

## 8 wajeruhiwa katika mlipuko Afghanistan

**KABUL,** AFGHANISTAN

Watu wanane wamejeruhiwa katika mlipuko wa bomu la kutupwa kwa mkono uliotokea katika shule ya dini ya Kiislamu katika mkoa wa Nangarhar mashariki mwa Afghanistan.

Maofisa walisema kuwa mlipuko huo umetokea usiku wa kuamkia jana katika wilaya ya Rodat na wanafunzi wawili miongoni mwa waliojeruhiwa walikuwa katika hali mbaya walipofikishwa hospitalini.

Hakuna madai ya watu waliohusika na shambulio hilo. Wanamgambo wa kundi linalojiita Dola la Kiislamu, IS, wamejikita nchini humo hasa eneo la mashariki, na mara kadhaa wamekuwa wakiendesha mashambulizi dhidi ya vikosi vya Taliban na vikundi vya kidini vya walio wachache.

Hivi karibuni, IS ilidai kuhusika na mashambulizi mawili tofauti dhidi ya kundi la Taliban mjini Kabul.

**DW**

# Mashambulizi ya makombora yaua 21 mkoa wa Odesa

**KYIV,** UKRAINE

WATU 21, akiwemo mtoto mmoja, wamefariki katika mashambulizi jana usiku yaliyofanywa na vikosi vya Russia katika eneo la Odesa kusini mwa Ukraine.

Kulingana na maofisa wa serikali wa huduma ya dharura (DSNS) walisema watu 16 waliuawa katika jengo la ghorofa tisa lililopigwa na kombora moja katika kijiji cha Serhiyivka.

Watu wengine watano akiwemo mtoto mmoja waliuawa katika eneo la mapumziko katika kijiji hicho. Russia ilirusha makumi ya makombora katika miji ya Ukraine katika siku chache zilizopita.

Juzi msemaji wa Ikulu ya Kremlin, Dmitry Peskov alikanusha tena kwamba nchi yake ilikuwa inalenga makazi ya raia.

"Tulisikia milipuko mitatu na sasa hakuna chochote kilichosalia kwenye kituo cha burudani," mkazi wa eneo hilo Yulia Bondar, aliiambia BBC. "Kijiji kiko kimya sana,hatukuwahi kufikiria kuwa hii inaweza kutokea." Aliongeza.

**UKRAINE YATAKA KUKAMATWA KWA MELI YA NAFAKA**

Ukraine imetoa wito kwa meli iliyobeba nafaka kutoka eneo linalokaliwa na Russia nchini humo kukamatwa.

Kwa sasa meli hiyo iko nje ya pwani ya Uturuki.

"Tumefuatilia meli yenye bendera ya Russia, Zhibek Zholy, kwenye njia yake kutoka bandari ya Berdyansk ya Ukraine hadi bandari ya Karasu ya Uturuki," ilisema taarifa hiyo.

Haijulikani shehena hiyo ya nafaka ilitoka wapi au ilipatikana vipi, lakini Russia imeshutumiwa kwa kuiba nafaka kutoka maeneo ya Ukraine inakodhibiti.

**WAINGEREZA WAWILI WALIOKAMATWA**

Raia wawili wa Uingereza wamekamatwa na vikosi vya Russia na wameshtakiwa kwa makosa ya kuwa mamluki wa kivita.

Dylan Healy, ambaye ni mpishi alikuwa akijitolea kama mfanyakazi wa misaada, alikamatwa katika kituo cha ukaguzi mwezi Aprili.

Siku hiyo hiyo, Russia ilitoa video ya Andrew Hill akiwa amevalia sare za kijeshi, akisema alikuwa amejisalimisha mwenyewe.

Taarifa hiyo inakuja baada ya wanaume wengine wawili wa Uingereza, Shaun Pinner na Aiden Aslin, kuhukumiwa kifo mwezi uliopita.

Healy na Hill wanakabiliwa na mashtaka sawa na hayo katika kesi iliyofunguliwa katika mahakama ya uwakilishi ya Russia mashariki mwa Ukraine, ambayo haitambuliki kimataifa.

Mahakama ya Ulaya ya Haki za Kibinadamu tangu wakati huo imeingilia kati kutaka hukumu hiyo isitekelezwe.

Lakini Russia imekataa wito huo, ikisema haitekelezi tena maamuzi ya mahakama ya Strasbourg na hatima ya watu hao ni suala la Jamhuri ya Donetsk inayounga mkono Russia.

**BBC**



Mvua zinazoendelea kunyesha katika nchi za India na Bangladesh zinasababisha athari kubwa, pichani ni barabara moja katika eneo la Sylhet, nchini Bangladesh,ikiwa imejaa maji. **PICHA: AFP**

# Mgao wa umeme waliza raia Afrika Kusini

**CAPE TOWN,** AFRIKA KUSINI

RAIA wa Afrika Kusini wanapambana kustahamili ongezeko la mgao wa umeme ulioathiri maisha na biashara nchini humo.

Nchi hiyo imeshuhudia mgao wa umeme kwa miaka kadhaa, lakini wiki hii shirika la umeme linalomilikiwa na serikali la Eskom limeongeza muda wa mgao hadi kupelekea baadhi ya wakazi na wafanyabiashara kukosa nishati hiyo kwa zaidi ya masaa 9 kwa siku.

Kulingana na wataalam, mgomo wa wafanyakazi wa Eskom uliongeza masaibu yanayoliandama shirika hilo ikiwa ni pamoja na kuharibika kwa mitambo yake michache na iliyochakaa ya nishati ya makaa ya mawe, uwezo mdogo wa uzalishaji na kukithiri kwa rushwa.

Kukatika kwa umeme kunawaathiri Waafrika Kusini walio wengi katika kipindi hiki cha baridi wakati familia nyingi zinategemea umeme kupasha joto majumba yao na kupika.

**DW**

MAKALA

# MWALIMU YUPI ALIYEFELI?



Na Magabilo Masambu - 0689157789

**Hivi hujawahi kuona mwanafunzi ametoka na 'division one' kidato cha nne akarudi na division zero kidato cha sita? Mada karibu zote za kidato cha sita si zile za kidato cha nne mfano kwenye Hisabati kidato cha nne tunasoma 2by2 matrix kidato cha sita ni 3by3 matrix, kidato cha sita kuna mada kama Complex number, Numerical Method, Calculus nakadhalika.**

KUNA dhana imejengeka katika nchi yetu kwamba wale wanaosomea ualimu ni watu waliofeli na kwamba chaguo la ualimu ni la mwisho baada ya kukosa kozi nyingine za maana kwa mujibu wa mtazamo wao. Mtazamo huu si wa siku nyingi sana kwa sababu miaka ya nyuma, hasa kutoka uhuru kazi ya ualimu ilionekana kazi ya maana kuliko kazi nyingine, ndiyo maana karibu wana mapinduzi na viongozi wengi walianza kuwa walimu.

Tunayo mifano ya baadhi ya viongozi wengi hapa Afrika ambao walianzia kwenye ualimu na baadaye kuwa viongozi wakubwa wa kitaifa. Wa kwanza kabisa ni Julius Kambarage Nyerere, wengine ni Robert Mugabe wa Zimbabwe, Kenneth Kaunda wa Zambia, Daniel Arap Moi wa Kenya, Mzee Ali Hassan Mwinyi, Dk. John Pombe Mgufuli, Waziri Mkuu wa sasa, Kassim Majaliwa hawa ni baadhi tu ya viongozi kati ya wengi ambao taaluma zao za kwanza ni ualimu. Je, nao kwao lilikuwa chaguo la mwisho?

Kazi ya ualimu wakati huo ilionekana ni ya maana sana, si kwa sababu nyingine yoyote bali walilipwa vizuri katika mishahara yao. Hii ina maana kwamba hata leo ikitokea mishahara ya ualimu ikazidi kada zingine zote itasalia kuwa kazi ya heshima.

Kwa hiyo, tatizo siyo ufaulu ndiyo maana kazi ya ubunge leo inaonekana ya maana kwa sababu wanalipwa vizuri huku sifa ya kupata kazi hiyo pamoja na vigezo vingine kama kuwa na dhamana ya chama cha siasa lakini zaidi ujue kusoma na kuandika, kazi yake ni kutunga sheria, kuikosoa, kuishauri na kuisimamia serikali!

Mwalimu yupi amefeli? Sifa ya mwalimu awe ama ana diploma au shahada maana yake wote hawa wamemaliza kidato cha sita, tafsiri yake ni kwamba wote walikuwa wanafunzi bora kidato cha nne, walifaulu mitihani na kujiunga kidato cha tano na hatimaye kidato cha sita, anaporudi kuja kufundisha masomo aliyoyafaulu unasemaje amefeli? Kusoma diploma au shahada (degree) maana yake amefaulu tena kidato cha sita kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa.

Elimu ya chuo kikuu. Sifa ya mwalimu awe na kuanzia shahada ya kwanza na kuendelea maana yake ni kwamba, mwalimu bora kabisa wa chuo kikuu ni mwanafunzi aliyefaulu vizuri sana katika masomo yake ya shahada ya kwanza, siyo mwenye shahada ya uzamili (master's degree) wala uzamivu (PhD) ndiyo maana wale ambao huwa wanafanya vizuri vyuo vikuu huwa wanabakizwa kufundisha na baada ya hapo wanaongezea mbwembwe zaidi lakini msingi wake ni shahada ya kwanza.

Kuna wakati unaweza kushangaa mwalimu ana shahada ya chuo kikuu lakini anashindwa kufundisha vizuri wanafunzi wa kidato cha kwanza maana yake mwalimu huyo ana shahada na ameifaulu vizuri lakini hakuwa vizuri katika masomo ya sekondari na hii ni kwa sababu kuna tofauti kubwa kati ya masomo ya ualimu wanayojifunza vyuoni na masomo ya taaluma.

Hapa ninamaanisha kwamba, kuna mtu anaweza kupata daraja sifuri kidato cha sita lakini akawa mwalimu mzuri sana kidato cha kwanza mpaka cha nne! Unashangaa?

Hivi hujawahi kuona mwanafunzi ametoka na 'division one' kidato cha nne akarudi na division zero kidato cha sita? Mada karibu zote za kidato cha sita si zile za kidato cha nne mfano kwenye Hisabati kidato cha nne tunasoma 2by2 matrix kidato cha sita ni 3by3 matrix, kidato cha sita kuna mada kama Complex number, Numerical Method, Calculus nakadhalika.

Changamoto za kufeli kwa wanafunzi tunahitaji kuzitatua siyo kukwepa kwa janja na kusingizia kwamba walimu wamefeli ndiyo maana hawafaulishi, hao wanaofaulu wanafundishwa na mizimu? Au ni walimu hawahawa waliofeli? Tunajaribu kutafuta dawa isiyo tiba.

Jambo la kusikitisha ni kwamba, kwa sasa mtazamo na msukumo wetu umekuwa ni juu ya kulenga matokeo makubwa badala ya kujenga maarifa na ujuzi, hatutatatua matatizo ya elimu nchini kwa kupanua elimu ya sekondari ili kila mmoja afike chuo kikuu na kujiita wasomi huku tukiwaita wanaotoa elimu hiyo kuwa wamefeli.

Jamii ya watu wajinga huwa haithamini elimu na kutothamini elimu kunaanza na kumpatia mwalimu majina ya kumdhalilisha huku ikitegemea matokeo makubwa yanayotokana na elimu hiyo. Hata wakoloni walianza kutuita majina mabaya ili tujione hatuna thamani baadaye wakatutawala, kama jamii kwa ujumla tunahitaji mtazamo mpya kabisa juu ya elimu yetu nchini.

Tuwatie moyo walimu, kazi wanayofanya haina mfano wake kwa sababu hakuna mtu anayejitapa na hasa kama anajua kusoma na kuandika kama hakupita kwa mwalimu.

Haya maneno tungetarajia kuyasikia kwa watu ambao hata kusoma na kuandika hawajui maana hawakufundishwa na mwalimu, hivyo hawajui umuhimu wake. Ebu jaribu kufikiria unampeleka mwanao shule hajui chochote kesho anakuwa daktari, mhandisi, rubani, mwanasheria nakadhalika, bado unasema huyu mwanangu amefundishwa na mwalimu aliyefeli, umeshindwa nini kuwa mwalimu wewe ili umfundishe mwanao?

**0689157789**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Super Rainbow, ilivyoibuka, kutoweka, sauti ya Sheggy ikichanganya wengi



Na Adam Fungamwango

MMOJA kati ya wasomaji wangu maarufu wa safu hii, Amani Balisidya, mtoto wa mwanamuziki marufu wa zamani na kiongozi wa bendi ya Afro 70, alinipigia simu na kuniomba ikiwezekana wiki moja niizungumzie bendi aliyoihusudu sana, Super Rainbow, ikiwa na maana upinde wa mvua.

Kwa heshima yake leo nitaizungumzia bendi hiyo iliyoibuka tu ghafla kama wingu la mvua angani, na kutoweka kama ilivyoibuka, ghafla tu. Iliyeyuka kama samli kwenye kikaango cha moto.

Bendi hiyo ambayo pamoja na kutokuwa na umri mrefu, lakini hadi leo hii ipo kwenye mioyo ya mashabiki wengi wa muziki wa dansi kutokana na kazi chache za kukumbukwa walizoziacha.

Bendi hii haikuzidi miaka miwili au mitatu tangu ianzishwe na kuvunjika. Ilianzishwa mwanzoni mwa miaka ya 1980 na kuvunjika katikati ya miaka hiyo. Ni bendi iliyorekodi nyimbo zake redio Tanzania (RTD) mara mbili tu, lakini hadi leo zimekuwa ni alama ya muziki wa dansi nchini, licha ya kuwa ilikuwa moja kati ya bendi zilizoitwa au kujiita ndogo.

Iliporekodi mkupuo wa kwanza tu sidhani kama ilibaki kuwa bendi ndogo. Inawezekana iliendelea kuwa bendi ndogo kutokana na si kati ya zile zenye majina makubwa, lakini ikaondokea kupendwa na wengi na kujizolea umaarufu kiasi hata ilipotoweka kwenye ulimwengu wa muziki walisikitika sana.

Ni mambo mawili tu ambayo yanaitambulisha bendi hii. Kwanza ni mwanamuziki na kiongozi upande wa uimbaji wa bendi hiyo, Eddy Sheggy, pamoja na wimbo wake alioutunga 'Milima ya Kwetu.'

Ukiizungumzia bendi hiyo bila kumzungumzia mwanamuziki huyo na wimbo wake huo, basi historia yako inakuwa haijakamilika na hata mtu hawezi kufahamu kuwa inayozungumziwa hapo ni Super Rainbow.

Mwanzoni mwa miaka ya 1980, RTD ilianza kupiga wimbo wa 'Milima Ya Kwetu', ambao kwa muda mfupi tu uliondokea kupendwa na mashabiki, ambao hawakuwa hata wanaifahamu bendi hiyo.

Sauti nyororo za waimbaji na mpangilio wake ulikuwa wa kipekee na haukuwa unafanana na bendi zingine za Tanzania. Na si bendi za wanamuziki wa Kitanzania, lakini hata bendi za hapa nchini zilizokuwa na Wakongomani, hawakuwa na aina hiyo ya uimbaji.

Baadhi wakadhani huenda wimbo huo umepigwa na bendi kutoka Kenya. Haikuwa hivyo.

Si wengi walidhania kuwa bendi hiyo ilikuwa na makao makuu yake maeneo ya Mwananyamala B, kwenye baa ya Sunlight, nyuma kidogo ya Shule ya Msingi Mwananyamala B, au Soko la Mwananyamala, maarufu kama Mapinduzi.

Ilikuwa na wanamuziki kama Hatibu Iteitei, Nuzi Ndoli, Rocky, Mzee Bebe na baadaye akaletwa Maneno Uvuruge. Duru za muziki zinasema hao ndiyo walioanzisha bendi, huku Eddy Sheggy na mkewe Emma Mkelo wakijiunga baadaye.

Muda mfupi baadaye wakaja wanamuziki wengine kama Banza Taxi, Nana Njige, Juma Choka, Rosh Mselela wakitokea Orchestra Mambo Bado ambayo ilikuwa imevunjika.

Inasemekana kifo cha Super Rainbow kilitokana na Tchimanga Kalala Asossa kuifufua upya Orchestra Mambo Bado na katika mpango wa kuwarudisha wanamuziki wake waliokwenda kwenye bendi hiyo, alisomba na wengine pia hadi kina Uvuruge.

Eddy hakuwepo kwenye mpango huo, hivyo baada ya bendi kusambaratika alikwenda kujiunga na African Sound 'Afriso Ngoma' iliyokuwa chini ya Lovy Longomba, lakini akadumu kwa kipindi kifupi kabla ya kuchukuliwa na Vijana Jazz Band. Hata wimbo wa 'Chaurembo' alikuwa ameutunga na kuuimba Afriso, lakini akahamia nao Vijana kabla ya kuurekodi.

Eddy, mzaliwa wa Tanga ndiye aliyekuwa staa kwenye bendi ya Super Rainbow, pamoja na kufanya muziki akiwa Tanga, lakini alikwenda nchini Kenya na kupiga bendi mbalimbali, ikiwemo Super Sound, ya Kalala Mbwebwe na kurekodi kibao ya 'Fanta'.

Inawezekana ikawa ndiyo sababu hata staili ya wimbo ya 'Milima ya Kwetu' kuonekana kama ni bendi ya Kenya.

"Nyimbo nyingine na Super Rainbow ni kama 'Kichekesho', 'Mateso', Milima ya Kwetu no 2', 'Kipaji Changu', 'Hesabu', 'Hidaya' na nyingine nyingi.

Sauti nyororo ya Eddy iliwachanganya wengi wakidhani ni ya mwimbaji wa kike. Na kwa sababu kulikuwa na kina Mkelo, na Njige, wengi walishindwa kuzitofautisha na hasa wale ambao hawakuwa wanakwenda kwenye maonyesho na kusikiliza kwenye redio.

Na hata waliokuwa wakiambiwa sauti hiyo ni Sheggy, basi walijua atakuwa na mwimbaji wa kike.

Utata wa Eddy sauti yake, anayeimba ni mwanaume au mwanamke, iliisha alipojiunga na Vijana Jazz.

Hapo ndipo wasioamini waliamini kuwa Eddy ni mwanaume, na ile sauti nyororo kama ya kike waliyokuwa wakiisikia Super Rainbow ni ya kwake, si ya Emma wala Njige. Wao walikuwa waitikiaji tu.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

PRINCE Petit kijana aliyelelewa kwenye mazingira ya ajabu. Amelelewa na baba yake mzazi tu bila mama. Madada wa kazi waliopewa kazi ya kumlea walipewa mkataba wa mwaka mmoja mmoja tu na wanapomaliza hawakuongezwa. Hakupelekwa shule yoyote ile, badala yake walimu walilipwa pesa kwa ajili ya kumfundisha nyumbani tu. Hata alipokuwa akipata nafasi ya kwenda kufurahia maisha na kuitazama dunia nje ya nyumba yao, alipewa angalizo la kutozoena na mtu yeyote yule. Aliingiziwa falsafa na vitu vingine kichwani mwake mpaka akawa na tabia ambazo ni tofauti na umri wake. Akiwa na miaka mitano tu, alianza kufundishwa kulenga shabaha na alipofikia miaka minane tu alikuwa na uwezo wa kutumia bastola ya aina yoyote ile na angeweza kuajiriwa kwenye shirika lolote la kijasusi duniani Anapofika umri wa miaka 25, baba yake mzee Pokwa anamtuma kazi. Kazi ya kuua na kulipiza kisasi. Ni kwa nini? Anakwenda kumuua nani? Kwa nini baba anayejua mkasa mzima asiende mwenyewe? Kitu gani kilichotokea huko nyuma? Nakala yako ya Nipashe itakufanya kujua kilichopo nyuma ya pazia.

# Mwisho wa Mauaji-8

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

DAKIKA moja iliyofuatia alirejea akiwa na picha mbili. Akampatia kijana wake.

"Hiyo picha namba moja ni ya jamaa mmoja anaitwa Nassor, na hiyo namba mbili ni Nassir. Hawa ni mapacha. Nao pia wameshiriki mauaji ya mama yako mzazi, hawatakiwi kuishi."

Baada ya kuongea hivyo alimtazama kijana wake halafu akaendelea.

"Taarifa za udukuzi nilizozipata leo mchana ni kwamba kesho jioni watakuwa kwenye harusi maeneo ya Tuangoma, Kigamboni.

Nasema hivi kwa sababu kama utachanga karata zako vizuri, unaweza kuwamaliza wote wawili kwa wakati mmoja. Ni kwa sababu watakuwa kwenye gari moja."

"Du, baba hizi taarifa zao huwa unazipataje?" Prince akashangaa.


"Nina vyanzo vyangu mimi, ingawa havijui kuwa nataka kujua habari zao kwa sababu ya kuwamaliza."

"Enhee baba endelea."

"Sasa mwanangu, yaani ni kwamba mmoja anajua kuendesha gari na mwingine hajui, kwa hiyo huwa mara nyingi wanakuwa kwenye gari moja. Ni kama vile mmoja anamuendesha mwenzake kwa sababu yule Nassir ndiye mwenye gari na tajiri, lakini hajui kuendesha. Pacha mwenzake Nassor ndiyo kama dereva wake. Ni harusi ya ndugu yao, watakuwa hivyo. Kama utaifanya kazi hiyo kabla ya harusi au baada hiyo ni shauri yako. Mimi nachotaka kusikia hapa kesho kutwa ni kwamba wamekwenda na maji. Nilichokufundisha ni ujasiri na kulenga shabaha, hilo peke yake linatosha, mengine utajiongeza mwenyewe kulingana na mazingira." Pokwa akawa anatoa ramani ya vita.

"Sawa baba kama ni hivyo niachie mimi nachotaka kujua harusi itaanza saa ngapi na hoteli gani."

"Saa 12 jioni hadi saa sita kwenye hoteli ya Camel, Tuangoma Kigamboni. Wao ni ndugu wa huyo dada anayeolewa, ukifika kwenye kituo cha daladala kinaitwa 'kwa fundi basikeli' basi mtu yoyote ukimuuliza atakuonyesha kwa sababu si mbali sana na hapo."




**"Saa 12 jioni hadi saa sita kwenye hoteli ya Camel, Tuangoma Kigamboni. Wao ni ndugu wa huyo dada anayeolewa, ukifika kwenye kituo cha daladala kinaitwa 'kwa fundi basikeli' basi mtu yoyote ukimuuliza atakuonyesha kwa sababu si mbali sana na hapo."**

"Nimekuelewa baba, ila ninachotaka hapa ni kitu kimoja tu ili nirahisishe kazi. Naomba aina ya gari na namba yake ya usajili. Unajua pamoja na picha zao, lakini kuhangaika kutazama sura zao mpaka kuzigundua mbele ya watu wengine namna hiyo halafu usiku ni ngumu sana. Mpaka uwatambue, halafu uwe na uhakika kama ni wao, uwaangalie wanakwenda kupanda gari gani, ni shida kidogo. Nachotakiwa kujua gari lao ni lipi basi, sina haja tena ya kuhangaika." Prince alitoa wazo kwa baba yake ambaye alikuwa anatingisha kichwa kuonyesha kukubaliana naye kabla hajasema neno lolote.

"Kweli umeiva mwanangu. Ila angalizo ni kwamba tukimaliza kulipiza kisasi usijihusishe tena na kazi hii, hata kama itakuwa ni kama imekupendeza. Kumbuka sisi tunalipiza kisasi tu, hatufanyi kwa maslahi. Ndiyo maana nilikupiga marufuku kutochukua pesa yoyote ya mzee Hussein ulipokuwa unajiandaa kwenda kummaliza." Akaonya mzee Pokwa.

"Hilo halina shaka, nikimaliza nitakuwa mtu mwema tu."

******************************

Kama alivyotegemea, kulikuwa na idadi kubwa ya magari nje ya hoteli ya Camel ambako ndiko sherehe za harusi zinafanyika.

Ni hoteli ya kisasa haswa, iliyostahili kuitwa hivyo. Siku hiyo aliamua kwenda na pikipiki, kwenye jumba ambalo anakaa peke yake, na baba yake huja mara moja moja, kuna gari moja na pikipiki ambazo zote amepewa kwa matumizi yake.

Alijua kazi anayokwenda kuifanya ni tofauti na ile ya mwanzo. Ni ya kuwaondoa wawili kwa wakati mmoja. Na hiyo itawezekana tu kama watakuwa wote ndani ya gari. Kwa hiyo akaona yeye hahitajiki kuwa na gari, bali pikipiki ambayo itamrahisishia kazi.

Alifika hapo saa mbili, kwa sababu aliambiwa itaanza saa 12:00 jioni hadi saa sita usiku.

Hakuna aliyemshuku kwani wengi walijua ni dereva wa bodaboda kama walivyo wengine. Alikwenda kusimamisha jengo la tatu kutoka hapo.

Na kwa bahati nzuri ilikuwa ni baa ya kawaida na nje walisimama watu wengi ambapo baada ya kufika hapo aligundua kuwa walikuwa wanaangalia mpira.

Pia aligundua walikuwa hapo nje walikuwa wakiangalia bure, lakini ukiingia ndani unalipia kinywaji.

Akaamua kujiunga nao. Hata hivyo hakuwa mmoja wa waliokuwa wanaangalia mpira usiku huo.

Akili na macho yake yalikuwa kwenye jengo la Camel Hotel kuangalia mwisho wa sherehe hizo za harusi.

Ilipotimu saa sita na dakika ishirini ndipo alipoanza kuona watu wanaanza kutoka. Haraka alichukua pikipiki lake na kusogea karibu na wahudhuriaji, kana kwamba anataka kuchukua wateja. Lengo lake ni kuwaona kwa karibu anaowawinda. Hakuwaona.

Alijitahidi sana kuangaza huku na huko. Akakumbuka kuwa alipewa karatasi ya aina ya gari na namba za usajili. Hii aliona itamsaidia zaidi kuliko kuanza kuangalia watu ambao wapo kwenye kundi la watu.

Aliangaza huku na huko, mwishoni kwenye kona ya jengo hilo aliliona gari alikokuwa akilihitaji.

Lilikuwa ni Toyota Premio rangi ya kijivu, ambalo lilikuwa na namba zinazofanana na zile alizopewa na mzee Pokwa kwenye kikaratasi chake. Alitabasamu. Sasa macho yake aliacha kuelekeza kote, bali kwenye gari ile tu. Dakika ishirini na tano baadaye akamuona mmoja wa watu anaowasaka. Hakujua kama ni Nassor au Nassir, lakini kwa jinsi sura ilivyo hakuhitaji hata kuangalia picha aliyopewa na baba yake kuthibitisha kuwa ndiyo mmoja wao.

Wakati akidhani labda mmoja wao hakuja kwenye sherehe hizo kwani tayari yule aliyekuja alikuwa ameshawasha gari na kugeuza, akamuona mwenzake akilifuata. "Kazi imekamilika." Akajiambia mwenyewe.

Alipohakikisha wote wameingia kwenye gari akajipigia makofi kimoyomoyo. Hakuwa na haraka, aliiacha itangulie na yeye kuanza kuifuata kwa mbali.

Bahati nzuri aliyoipata ni kwamba magari mengi yalikuwa yameshatangulia kuondoka. Gari la Nassor na Nassir yalikuwa ni kati ya yale machache yaliyobaki.

Aliwasha pikipiki yake na kuanza kuifuata kwa kasi. Kila kitu alishakipanga na mpaka eneo la kufanya tukio.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# TICHA STAR
## Mhadhiri UDOM anayeng'ara katika muziki

WAKATI akifundisha darasani hautafikiria kwamba unaweza kumkuta akiwa juu ya jukwaa la muziki akiimba na kucheza kama ilivyo wasanii wengine.

Kwa wanafunzi wanaosoma Chuo Kikuu cha Dodoma, wanamjua kwa jina la Ticha Star, si tu kutokana na umahiri wake wa kuwafundisha wanafunzi, bali ni kipaji chake kingine cha kuimba na kucheza muziki.

Jina lake halisi ni Dk. Meserecordias Wilfred Lema, mzaliwa wa Kilimanjaro.

Msomi huyo wa Shahada ya Uzamivu (yaani PhD), katika Uhandisi wa Mazingira, pia ni ni mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

Kwa sasa Ticha Star anatamba na kibao chake kinachoitwa 'Ukinipenda'chenye maadhi ya Rhumba.

Ticha Star ni mwanamuziki wa muziki wa majukwaani, yaani 'live band' na amepata umaarufu katika jiji la Dodoma kutokana na kazi yake hiyo ya sanaa.

Anasema ameimba majukwaani kwa muda wa zaidi ya miaka mitano, kabla ya kuamua kuingia studio kurekodi wimbo wake wa kwanza.

Wimbo huo 'Ukinipenda' ameurekodi katika studio ya Trace Records zilizopo jijini DODOMA.

Ticha star anaeleza alianza kupenda muziki toka akiwa mdogo, ambapo alianza kuimba kwaya katika kanisa la Tanzania Assemblies of God, kijijini Machame.

"Naweza kumudu majukumu yangu yote mawili kufundisha na muziki, kwa sababu vyote viwili ni vipaji nilivyopewa na Mungu," anasema Ticha Star.

Anasema mipango yake katika muziki ni kuufanya muziki wa dansi usikike zaidi, ndani na nje ya mipaka ya Tanzania, kwa kutoa nyimbo nyingi, nzuri na zenye kuvutia.

Anasema style yake ya muziki inaitwa 'Dance Flavour' kutokana na kuchanganya vionjo vya muziki wa dansi na miziki mingine kama Bongo Fleva, Amapiano na muziki wa Afrika Magharibi.

Anamalizia kwa kusema, yeye anapatikana katika mitandao yote ya kijamii, mfano twitter, instagram, youtube, facebook nk., kwa jina la Tichastar.

# Shilole unataka kumtibua Baba levo

MWAMUZIKI wa Bongo Fleva, Shilole amesema rafiki yake wa muda mrefu Babalevo,baadhi ya watu walikuwa wanamkataa kwa sababu alikuwa anaomba omba sana.

Akielezea ukaribu wake na Babalevo kupitia DADAZ ya East Africa TV, Shilole amesema kuna wakati lazima awe mkweli amekuwa amkimshika mkono kwa muda mrefu kutokana na tatizo lake hilo.

"Maji yakinifika hapa huwa namchana ukweli Babalevo ila sisi ni washkaji sana, unaweza kutuona mitandaoni tunachambana lakini baadaye ananiomba elfu 20". Amesema Shilole.



## ZISIKUPITE

### ERIKSEN ATAKIWA

KLABU ya Manchester United inakaribia kumsajili kiungo wa Denmark, Christian Eriksen baada ya mkataba wake katika klabu ya Brentford kuisha. ***(Star)***

### DEMBELE AGOMBEWA

KLABU za Chelsea, Paris St-Germain na Bayern Munich zinapigania kumsajili mshambuliaji wa Barcelona na Ufaransa, Ousmane Dembele, 25, huku mchezaji huyo akipatikana kwa uhamisho wa bila malipo. ***(Marca)***

### DENNIS AWANIWA

MSHAMBULIAJI wa Watford na Nigeria, Emmanuel Dennis, 24, ni miongoni mwa wachezaji wanaolengwa na Everton. ***(Evening Standard)***

### ASENSIO KUONDOKA

KIUNGO wa Real Madrid na Hispania, Marco Asensio, 26, huenda akaondoka katika uwanja wa Bernabeu mwishoni mwa msimu huu. AC Milan ni miongoni mwa timu zinazomnyatia mchezaji huyo. ***(Marca)***

### LINAGARD ATAKIWA

KLABU ya Tottenham Hotspur imejiunga na West Ham, Everton na Newcastle katika kufikiria kumsajili kiungo wa kati wa England, Jesse Linagard, 29. ***(Telegraph)***

### EKITIKE KUBAKI

MSHAMBULIAJI wa Reims, Hugo Ekitike, 20, ameiambia klabu hiyo ya Ligue 1 kuwa anataka kusalia. ***(Mirror)***

### LENGLET HUYO SPURS

KLABU ya Tottenham hotspur inakaribia kumsajili beki wa Barcelona na Ufaransa, Clement Lenglet, 27. ***(Express)***

### DOUCOURE KUTUA PALACE

KLABU ya Crystal Palace inakaribia kumsajili kiungo wa kati wa Lens, Cheick Doucoure katika makubaliano yenye thamani ya euro milioni 21 pamoja na marupurupu kwa mchezaji huyo wa Mali mwenye umri wa miaka 21. ***(Guardian)***

### PEREIRA KUBAKI FLAMENGO

FULHAM imeruhusiwa kuzungumza na kiungo wa kati wa Brazil, Andreas Pereira, 26, baada ya kukubaliana dau na Manchester United, kiungo huyo anataka kubakia katika timu ya Flamengo ya nchini Brazil ambapo yupo kwa mkopo. ***(90 Min)***

### BROWNHILL ATAKIWA

KLABU ya Southampton imejiunga kwenye mbio za kuwania kumsajili kiungo wa kati wa Burnley na England, Josh Brownhill, 26. ***(90 Min)***

### EDOZIE KUUZWA

MANCHESTER City imekubali kumuuza mchezaji wa England anayechezea timu ya wachezaji wasiozidi umri wa miaka 19, Sam Edozie, 19, kwa klabu ya Ujerumani ya Bayer Leverkusen kwa dau la pauni milioni 10. ***(Football Insider)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# PSG SASA YAFIKIRIA KUMUUZA NEYMAR

## ●●● Bado hawana uhakika kama wamuuze kabla ya kombe la Dunia au baada...

**PARIS,** Ufaransa

WAMILIKI wa Paris Saint-Germain hawana uhakika kama kumuuza Neymar kabla ya Kombe la Dunia ni jambo sahihi kufanya, kwa mujibu wa 90min.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 alitia saini mkataba mpya katika klabu hiyo ya pale Parc des Princes mwaka jana, akipokea kiasi cha euro milioni 43 kila mwaka na bonasi, na muda wake hapo unamalizika mwaka 2027.

Uongozi wa klabu hiyo uko tayari kufurahia matarajio ya Neymar kuondoka, huku Kylian Mbappe akichukua nafasi ya uongozi katika timu hiyo yenye maskani yake mji mkuu wa Ufaransa baada ya kukataa kwenda Real Madrid.

**Rais wa klabu hiyo, Nasser Al-Khelaifi juzi alikataa kuthibitisha kwamba Neymar atasalia Paris zaidi ya msimu huu wa joto, akionya kwamba PSG inaweza kuwaachia wachezaji kadhaa.**

Lakini kwa mujibu wa 90min wamiliki wa PSG kutoka nchini Qatari hawaamini kwamba kumwacha Neymar aondoke kabla ya Kombe la Dunia la 2022 ni jambo sahihi kufanya, na wanataka kutathmini hali kikamilifu kabla ya kufanya uamuzi.

Wakati huo huo, 90min inaelewa kuwa wamiliki hao wameziarifu klabu nne za Ligi Kuu England Manchester United, Manchester City, Chelsea na Newcastle United kuhusu uwezekano wa kupatikana kwa Neymar.

Bayern Munich, Juventus na Milan pia zimeonesha nia ya kutaka huduma ya mchezaji huyo.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
ZENIT ST PETERSBURG
VERSUS
RED STAR BELGRADE
1 | 1.71
X | 3.53
2 | 4.32

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MAN UNITED YATOA OFA KWA MARTINEZ

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imetoa ofa ya euro milioni 43, ambayo huenda ikapanda hadi euro milioni 45 kwa mabingwa wa Uholanzi Ajax ili kumsajili, Lisandro Martinez.

United wameelekeza nguvu zao kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina baada ya kuwa kwenye nafasi nzuri ya kumsajili, Frenkie de Jong kutoka Barcelona na Tyrell Malacia wa Feyenoord.

Kwa mujibu wa 90min Martinez ndiye mlengwa mkubwa kwa Man United huku kocha, Erik ten Hag akitaka kumleta mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 pale Old Trafford huku pia Arsenal wakimtaka.

Inafahamika ofa rasmi sasa imetolewa na United, yao ni kubwa kuliko ofa mbili za awali za Arsenal.

Ajax wanadaiwa kumthamini mchezaji huyo kwa karibu euro milioni 50, lakini United wanatumaini kuwa dili linaweza kufikiwa.

United wanaamini kabisa mchezaji huyo angependa kuhamia Old Trafford na sasa wamewatangulia Washikabunduki katika mbio za kumuwania beki huyo, ambaye anaweza kucheza beki wa kati na kushoto.

United kwa hakika wana matumaini kwamba, wanaweza kuwa na wachezaji wengi waliosajiliwa wapya wakati watakapoondoka kwenye ziara yao ya maandalizi ya msimu mpya nchini Thailand na Australia.






## Juventus yamtaka Pulisic

**TURIN,** England

KLABU ya Juventus imeifahamisha Chelsea kwamba, watakuwa tayari kumpokea Christian Pulisic kama sehemu ya kumuuza beki wa kati, Matthijs de Ligt.

Mmiliki mpya wa Chelsea,Todd Boehly yuko tayari kumpatia fedha za usajili kocha Thomas Tuchel ili aimarishe kikosi chake msimu huu wa joto na De Ligt sasa ameibuka kama shabaha yao kuu kwenye safu ya ulinzi.

Mholanzi huyo ameshindwa kukubaliana na masharti ya kuongezwa mkataba kule Juventus na anadaiwa kutaka kuzungumza na Chelsea.

Juventus wanasitasita kumpoteza De Ligt, lakini wanakubali kwamba mauzo yake yanaweza kuwa na faida kubwa.

Chelsea wako tayari kumtoa Pulisic msimu huu wa joto na pia wamebainisha kuwa Timo Werner anapatikana kwenye majadiliano pia.

Juventus wamethibitisha kuwa wako tayari kwa mabadilishano na ofa kutoka kwa Chelsea inatarajiwa kuwasili siku zijazo.

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# KOCHA PRISONS AIPIGIA HESABU MTIBWA SUGAR

**Na Cheji Bakari,** Tanga

KOCHA Msaidizi wa Tanzania Prisons, Shabani Mtupa amesema kuwa sasa wanajipanga katika hatua ya mchezo wa mtoano dhidi ya Mtibwa Sugar ili kujinusuru na kushuka daraja.

Prisons imeingia katika hatua hiyo baada ya kufungwa bao 1-0 na Ruvu Shooting katika mechi ya mwisho ya Ligi Kuu Bara ambapo imemaliza katika nafasi ya 14 ikiwa na jumla ya alama 29 ambapo ipo katika mstari wa njano wa kucheza hatua ya mtoano sambamba na Mtibwa Sugar ambayo imemaliza ligi ikiwa katika nafasi ya 13 ikiwa na alama 32.

**"Hapa tulipo tumejipanga kuhakikisha tunashinda mchezo wetu dhidi ya Mtibwa ili kujihakikishia nafasi ya kubaki Ligi Kuu," amesema Mtupa.**

Julai 6 itacheza tena Manungu, Morogoro ambapo mshindi wa jumla atapanda moja kwa moja Ligi Kuu Bara.

Timu itakayoshindwa itapata nafasi nyingine ya kucheza na timu ya Ligi ya Championship ambayo ni JKT Tanzania FC.

JKT Tanzania ambayo ilishika nafasi ya tatu katika Ligi ya Championship pamoja na Kitayosce FC ya Tabora zilipata nafasi ya kucheza hatua ya mtoano baada ya JKT Tanzania ilishinda mechi zote.



Askari wa Jeshi la Kujenga Taifa JKT, wakitoa Burudani mbele ya banda lao katika maonyesho ya 46 ya Kimataifa ya Sabasaba barabara ya Kilwa, Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Pluijm kocha mkuu Singida Big Stars*



**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Singida Big Stars umemalizana na makocha wawili, Hans Pluijm kuwa mwalimu Mkuu akisaidiana na Mathias Lule kwa ajili ya kukinoa kikosi cha timu hiyo kwa msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Pluijm aliwahi kuzifundisha Yanga na Singida United misimu tofauti na Lule alikuwa kocha Mkuu wa Mbeya City msimu huu.

Taarifa za uhakika zilizolifikia gazeti hili kutoka ndani ya bodi ya wakurugenzi wa Singida Big Stars, ilisema makocha hao wameingia makubaliano ya mkataba wa mwaka mmoja kukinoa kikosi cha timu hiyo.

Kigogo huyo ambaye hakutaka kuweka wazi jina lake alisema Pluijm anatarajia kutua nchini Julai 10 kwa ajili ya kuanza kazi rasmi ya kujiandaa vema kwa msimu ujao wa mashindano yaliyopo mbele yao ikiwemo Ligi Kuu.

Alisema wanatambua mchango na uwezo wa makocha hao katika kazi yao baada ya mafanikio waliyoyapata katika timu walizofundisha kwa kuonyesha ushindani mkubwa katika Ligi ya Tanzania.

Wakati huo huo, Singida Big Stars jana imemtambulisha beki wa Yanga, Paul Godfrey ambaye amesaini mkataba wa miaka miwili kuimarisha kikosi cha timu hiyo kwa msimu ujao wa Ligi hiyo.

Singida Big Stars inatarajia kuingia kambini Julai 15 au 20, mwaka huu na mazoezi wataanza Mkoani Singida, baadae benchi la ufundi litakaloongozwa na Pluijm kupendekeza nchi atakayokwenda kufanya maandalizi ya msimu ujao wa Ligi hiyo.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 03/07/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1705 | Vasteras SK vs IK Brage | 2.12 | 3.61 | 3.20 |
| 14:00 | 4107 | Seoul E Land vs Jeonnam Dragons | 2.19 | 3.19 | 3.04 |
| 14:30 | 2874 | Shandong Luneng vs Guangzhou RF | 1.06 | 8.42 | 28.39 |
| 14:30 | 5945 | Wuhan Three Towns FC vs Shanghai Shenhua | 1.62 | 3.74 | 4.62 |
| 15:00 | 5594 | Hangzhou NG vs Henan Jianye | 3.39 | 3.10 | 2.07 |
| 15:15 | 4174 | Negeri Sembilan vs Sabah | 2.18 | 3.24 | 3.00 |
| 16:00 | 2540 | Mjondalen vs Stabaek | 3.04 | 3.39 | 2.10 |
| 16:00 | 2685 | Skeid Fotball vs Grorud IL | 1.91 | 3.68 | 3.29 |
| 16:00 | 2845 | Vitebsk vs Dinamo Brest | 2.01 | 3.20 | 3.45 |
| 16:00 | 3037 | Varbergs Bois vs IFK Varnamo | 2.52 | 3.06 | 2.66 |
| 16:00 | 3184 | AFC Eskilstuna vs Brommapojkarna | 2.96 | 3.77 | 2.19 |
| 16:00 | 3979 | Djurgardens IF vs Hammarby | 2.25 | 3.24 | 2.89 |
| 16:00 | 4240 | Kfum Oslo vs Sogndal | 1.92 | 3.58 | 3.33 |
| 16:00 | 4765 | Terengganu vs Pahang FA | 1.53 | 4.02 | 5.09 |
| 16:00 | 5599 | Astana vs Maktaaral | 1.21 | 5.51 | 10.83 |
| 17:00 | 4023 | Avai vs Cuiaba MT | 2.11 | 2.95 | 3.49 |
| 17:00 | 5536 | Ponte Preta vs Tombense MG | 2.10 | 2.84 | 3.68 |
| 17:55 | 4572 | Futbolo Akademija Siauliai vs Dziugas | 1.73 | 3.39 | 4.42 |
| 18:00 | 2176 | FK Tukums 2000/Tss vs FS Metta/Lu | 2.79 | 3.38 | 2.24 |
| 18:00 | 2290 | Kairat Almaty vs Akzhaiyk Uralsk | 1.50 | 3.78 | 5.89 |
| 18:00 | 4896 | Aksu vs FK Kyzylzhar Petropavlovsk | 2.50 | 2.99 | 2.74 |
| 18:00 | 5335 | BATE Borisov vs Energetik Bgu Minsk | 1.47 | 4.11 | 5.68 |
| 18:30 | 3850 | BK Hacken vs Elfsborg | 2.31 | 3.44 | 2.65 |
| 18:30 | 5906 | Norrkoping vs Sirius FK | 1.45 | 4.30 | 5.67 |
| 19:00 | 1612 | Ham-Kam vs Molde | 3.26 | 3.66 | 2.02 |
| 19:00 | 2609 | Kristiansund vs Lillestrom | 3.53 | 3.53 | 1.97 |
| 19:00 | 3790 | Sarpsborg vs Sandefjord | 1.43 | 4.61 | 6.22 |
| 19:00 | 4088 | Aalesunds vs Stromsgodset | 2.22 | 3.42 | 3.01 |
| 20:00 | 2662 | UNAM Pumas vs Club Tijuana | 1.91 | 3.42 | 3.87 |
| 20:00 | 2751 | Zenit St Petersburg vs Red Star Belgrade | 1.71 | 3.53 | 4.32 |
| 20:00 | 3089 | Gomel vs Neman Grodno | 3.19 | 3.14 | 2.14 |
| 20:00 | 4434 | Carlos Mannucci vs Sporting Cristal | 3.83 | 3.54 | 1.80 |
| 21:00 | 4575 | Viking vs Rosenborg | 1.79 | 3.77 | 3.97 |
| 22:00 | 1178 | Atletico GO vs Sao Paulo | 2.74 | 2.93 | 2.54 |
| 22:00 | 1503 | Vasco da Gama vs Sport Recife | 1.95 | 2.85 | 4.22 |
| 22:00 | 1589 | La Serena vs O Higgins | 2.49 | 3.13 | 2.64 |
| 22:00 | 2186 | Mirassol SP vs Uniclinic CE | 1.41 | 4.20 | 7.40 |
| 22:00 | 3082 | Chaco For Ever vs Mitre SdE | 2.16 | 2.95 | 3.34 |
| 22:00 | 3578 | Santamarina vs Tristan Suarez | 2.65 | 2.84 | 2.70 |
| 22:00 | 5419 | Bahia BA vs Gremio | 2.54 | 2.83 | 2.83 |
| 22:00 | 5473 | CA Guemes vs Deportivo Maipu | 3.30 | 2.96 | 2.18 |
| 22:15 | 4500 | Keflavik IF vs Fram Reykjavik | 2.00 | 3.57 | 3.13 |
| 23:00 | 1490 | Cavaliers FC vs Waterhouse FC | 2.80 | 3.43 | 2.22 |
| 23:00 | 1600 | CA Atlanta vs Instituto Cordoba | 2.85 | 2.80 | 2.55 |
| 23:00 | 1823 | Remo PA vs Paysandu PA | 2.55 | 3.04 | 2.65 |
| 23:00 | 1864 | Forge FC vs Atletico Ottawa | 1.68 | 3.53 | 4.52 |
| 23:00 | 3469 | Alianza Atletico vs FBC Melgar | 3.34 | 3.39 | 1.98 |
| 23:00 | 4273 | 12 de Octubre de Itaugua vs Club General Caballero Jlm | 2.75 | 3.15 | 2.39 |
| 23:00 | 4904 | Asociacion Deportiva Tarma vs Alianza Lima | 3.15 | 3.05 | 2.20 |
| 23:00 | 5715 | Sport Boys Association vs Sport Huancayo | 3.39 | 3.34 | 1.98 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumapili Julai 3, 2022
Nipashe



PSG kumuuza Neymar
UKURASA 21




Nahodha wa Yanga, Bakari Mwamnyeto akiwa amenyanyua juu kombe la FA walilolitwaa jana baada ya kuifunga Coastal Union kwa penalti 4-1 kwenye uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha. **PICHA: YANGA**

# Yanga bingwa FA

**Na Adam Fungamwangwo**

## ●●● Baada ya mechi kali ya kuvutia na kibabe, yaitungua Costal kwa...

MABINGWA wa Tanzania Bara, Yanga, jana waliongeza taji lingine kibindoni, ilipofanikiwa kuchukua pia Kombe la Shirikisho la Soka Nchini, FA, kwa kuiondosha Coastal Union kwa mikwaju 4-1 ya penalti, baada ya dakika 120 za jasho, machozi na damu, timu hizo zikitoka sare ya mabao 3-3 kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid Arusha.

**Yanga imetwaa kombe hilo baada ya misimu mitano kwani mara ya mwisho ilikuwa ni msimu wa 2015/16, ikifunga Azam mabao 3-1 Mei 26, 2016 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.**

Waliofanikisha mikwaju ya penalti kwa upande wa Yanga ni Yannick Bangala, Dickson Job, Heritier Makambo na Khalid Aucho, huku penalti pekee kwa Coastal Union ikifungwa na Victor Akpan, huku Amani Kyata na Rashid Chambo wakikosa penalti zao.

Mechi hiyo ililazimika kwenda kwenye mikwaju ya penalti baada ya kumalizika kwa dakika 120 zikiwa sare ya mabao 3-3.

Mtokea benchini, Denis Nkane aliipatia Yanga bao la kusawazisha dakika chache tu kabla mechi hiyo kumalizika, Coastal ikiwa mbele kwa mabao 3-3. Ilikuwa ni 'hat-trick' ya Abdul Selemani 'Sopu', akiifungia Coastal Union mabao yote, Feisal Salum, Makambo, na Nkane wakiifungia Yanga.

Matokeo hayo yalikuwa yakisubiriwa kwa hamu kubwa na Geita Gold, kwani sasa ndiyo itakayoiwakilisha Tanzania kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, ikiwa pamoja na Azam, huku Yanga na Simba zikienda kucheza Ligi ya Mabingwa.

Yanga ilianza kwa mashambulizi mfululizo langoni mwa Coastal Union na nusura wapate bao dakika ya tano tu, pale Feisal Salum alipoachia shuti lililowababatiza mabeki na kuzua kizaazaa, kabla ya kuokolewa. Shambulio la kwanza tu la Coastal Union ambalo lilikuwa la kustukiza lilizaa bao dakika ya 10 lililofungwa na mchezaji wao tegemeo, Sopu.

Alikuwa ni winga wa kulia Vicent Aboubakar aliyeondoka na mpira pembeni mwa uwanja, akimuacha Farid Mussa na kupiga krosi iliyomkuta mfungaji akiwa hajakabwa vema na Dickson Job, akaujaza wavuni.

Baada ya bao hilo ni kama Yanga ilihamia kwenye lango la Coastal, kwani ilifanya mashambulizi mengi, matatu yakiwa ya hatari ambayo yalifanywa na Fiston Mayele.

Dakika ya 14 aliwazidi mbio mabeki na kuachia shuti kali lililokwenda nje, lakini dakika moja baadaye aliupata mpira akiwa mita 35, akaachia 'mashine' iliyokwenda kugonga mwamba wa juu na kutoka nje.

Mayele tena akiwa hatua tatu tu kutoka langoni mwa Coastal Union, alikosa bao na kupiga mpira nje dakika ya 19 ya mchezo.

Dakika tano kabla ya kwenda mapumziko, Coastal nusura wapachike bao la pili baada ya Victor Akpan kummegea pande safi Moubarack Amza, ambaye aliachia kombora lililompita kipa Djigui Diarra, lakini badala ya kujaa wavuni, ukatoka sentimita chache langoni mwa Yanga.

Kipindi cha pili baada ya Yanga kufanya mabadiliko kwa kutoka Chico Ushindi na kuingia kwa Heritier Makambo kuliwapa uhai. Yanga ilisawazisha bao dakika ya 56 kupitia kwa Feisal Salum kwa shuti kali la mguu wa kushoto.

Alikuwa ni Makambo aliyeambaa kwenye winga ya kushuto na kupiga krosi iliyokuwa ikizagaa, ikamkuta mfungaji aliyeachia shuti lililowainua mashabiki wa Yanga waliokuwa uwanjani na vibanda umiza.

Baada ya kosa za hapa na pale, dakika tisa kabla dakika 90 kumalizika, Makambo aliukuta mpira uliookolewa kizembe na Amani Kyata akaachia shuti lililodunda na kujaa wavuni, ukimpita Mussa Mbissa kwapani.

Hata hivyo, dakika tatu kabla dakika 90 kumalizika, Sopu tena aliwainua mashabiki wachache wa Coastal Union, alipouweka wavuni mpira kwa kichwa na kufanya dakika kumalizika kwa mabao 2-2.

Akafunga tena bao la tatu kwenye kipindi cha kwanza dakika za nyongeza, kabla ya Nkane kusawazisha dakika chache kabla ya dakika 120, akiirudisha Yanga mchezoni.

# Simba kushusha beki kama Inonga

**Na Adam Fungamwangwo**

KLABU ya Simba imesema inatarajia kusajili beki mwingine wa kati ambaye uwezo wake unalingana na Henock Inonga ambaye atakuja kusaidiana naye msimu ujao wa mashindano.

Meneja Habari na Mawasiliano, Ahmed Ally amesema wanakusudia kifaa hicho kwa ajili ya kuja kusaidiana na Inonga ambaye kwa msimu wa kwanza tu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara amekuwa gumzo, huku akiwa kwenye kinyang'anyiro cha kuwania beki bora wa msimu.

"Nawapongeza wachezaji wetu wote ambao wameingia kwenye kinyang'anyiro cha kuwania tuzo ya Ligi Kuu, ila naweza kusema kuwa beki wetu Inonga ambaye amewekwa kwenye kipengele cha beki bora, angeweza kuwa hata mchezaji bora wa msimu, jamaa anajua mpira, msimu wake mmoja tu ametikisa, sasa msimu ujao tunakuja na beki mwingine kama Inonga, tunataka tutikise Afrika," alisema Ahmed.

Aliwataka wanachama na mashabiki wa Simba wasiwe na wasiwasi kuhusu usajili kwani viongozi wao wanaifanya hiyo kazi, kwa hiyo kwa sasa wapumzike tu baada ya msimu kumalizika.

Simba imepoteza ubingwa wa Ligi Kuu mara ya kwanza msimu huu baada ya misimu minne, lakini pia Kombe la FA baada ya misimu miwili, hivyo wanachama na mashabiki wake wamekuwa wakishinikiza viongozi kufanya mabadiliko makubwa kwenye kikosi hicho, ikiwa ni pamoja na kusajili wachezaji bora na wenye uwezo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >